

**MAMA KIJACHO Magauni haya yanakufaa**

UKURASA 13




**Aubameyang atetewa kuhusu kutokufunga**

UKURASA 22

**MAISHA** Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*





Jinsi ya kutengeneza tomato sauce



**MAISHA NI NYUMBA**
Bustani hupendezesha nyumba ikipangiliwa vizuri

HARUSI




# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Oktoba 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580379

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI MAALUM

# Unywaji wa maji holela chanzo maradhi ya moyo

• **Madaktari** bingwa wadokeza kilichojificha, janga liko zaidi kwa watu wanaokaa ofisini... *Endelea uk.4*


**YALIYOMO**

UKURASA WA 3
**CHADEMA, ACT-WAZALENDO WAFANYA KAMPENI PAMOJA**

UKURASA WA 5
**BABA NA MWANAWE WAHUKUMIWA KIFUNGO JELA KWA KUMHONGA DC**


# Lissu alalama hujuma uchaguzi



UKURASA 2



Rais Dk. John Magufuli, akinong'onezwa jambo na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, wakati wa ufunguzi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro Leather Industries Co. Ltd, katika Gereza la Karanga, mjini Moshi. **PICHA: IKULU**

# Magufuli aapa CCM kurejesha jimbo lililokaa upinzani miaka 25

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



**MICHEZO** **YANGA SC MAJARIBUNI MWANZA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

## Ajali ya basi yaua 15, yajeruhi wengine 20

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WATU 15 wamefariki dunia na wengine 20 kujeruhiwa baada ya basi la Fly Emerates kuacha njia na kuanguka kwenye korongo katika eneo lenye mteremko mkali la Kumunyange, Ngara mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema gari hilo aina ya TATA, lenye namba za usajili T670 DKL, lilipata ajali jana saa 4:00 asubuhi baada ya kupata hitilafu katika mfumo wa breki na kuongeza mwendo.

Malimi alisema kutokana na mteremko mkali na kona, dereva wa gari hilo, Phares Faustine (32), alishindwa kulimudu.

Alisema gari hilo lilikuwa likitokea Ngara kwenda Bukoba mjini na kwamba miili ya watu watatu ambao ni James Eustace (26), Merchaes Kahigi (25) na James Elias (23), wote raia wa Burundi, imetambuliwa, huku mingine 12 ikiwa bado haijatambuliwa.

Kamanda Malimi alisema majeruhi wote 20 kati yao 13 wanaume, watoto watatu na wanawake wanne, wamelazwa katika hospitali za Murgwanza na Nyamiaga zote za wilayani Ngara.

"Kati ya majeruhi hao 20, majeruhi wanane ni raia wa Burundi na hali za baadhi yao ni mbaya na wengine wanaendelea vizuri," alisema Malimi.

Alisema kazi ya kutambua marehemu hao bado inaendelea na kwamba chanzo cha ajali hiyo kinaendelea kuchunguzwa ingawa uchunguzi wa awali umeonyesha ni kukatika kwa "propeller shaft".

# JPM aapa kuchukua jimbo lililokaa upinzani miaka 25

**Na Gwamaka Alipipi,**
KARATU

MGOMBEA urais, Dk. John Magufuli (CCM), amesema ni wakati mwafaka kwa wananchi wa Jimbo la Karatu kufanya uamuzi wa kuuondoa upinzani katika jimbo hilo uliodumu kwa miaka 25.

Alisema kama wameongozwa na kiongozi wa upinzani kwa miaka hiyo na hakuna maendelea waliyoyapata, sasa ni wakati mwafaka wa kumchagua mbunge kupitia CCM kwa miaka mitano ijayo. "Karatu kama mnataka mabadiliko, mleteni Danieli Awack, kama mmekaa kwa miaka 25, jaribuni kuja CCM kwa miaka mitano halafu mniulize," alitamba.

Dk. Magufuli alisema Mgombea Ubunge wa CCM, Awack, alikuwa ni mjumbe wa NEC na ni mkulima wa vitunguu, lakini amekuwa akipigwa vita kwa sababu hana elimu ya shahada.

"Ninahitaji mbunge atakayewatetea watu, kuwasemea shida zao, ambaye atakuwa kiunganisho kati ya wananchi na serikali. Sihitaji mtu mwenye 'degree' (shahada), kwani kuwasemea watu shida ya barabara lazima uwe na 'degree'?" Dk. Magufuli alihoji.

Mgombea huyo pia alimwagia sifa Balozi Wilbroad Slaa, akimwelezea kuwa ni kiongozi bora kutoka chama cha upinzani, mtu makini na mjenga hoja wakati wote akiwa Mbunge wa Karatu.

Alisema Dk. Slaa alikuwa mwadilifu, mzalendo wa kweli kwa taifa lake na kwamba yawezekana alikuwa hivyo kutokana na kazi yake aliyowahi kuifanya ya kuwa kiongozi wa dini.

"Kwenye upinzani kama kulikuwa na mtu ambaye alikuwa kiongozi bora kuwahi kutokea ni Dk. Slaa, kati ya wapinzani wazalendo nchini, Dk. Slaa ni nambari moja," Dk. Magufuli alisifu.

Alisema Dk. Slaa alikuwa mtu mstaarabu tofauti na wabunge wengine wa upinzani, akisisitiza kuwa hakuwahi kutoa kauli za matusi wala kuweka kibandiko mdomoni kama wanavyofanya wabunge wa upinzani.

"Baada ya kukaa upinzani na kuona ubabaishaji, akaamua kujitoa mwenyewe, nami kwa kutambua uwezo wake, nikamteua kuwa balozi katika nchi tisa," alisema.

Alifafanua kuwa Dk. Slaa kwa sasa anaiwakilisha Tanzania katika nchi za Sweden, Norway, Denmark, Island, Finland, Ukraine, Lativia, Estonia na Lithuania.

Dk. Magufuli pia alisema katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imejenga Hospitali ya Wilaya Karatu na upanuzi wa Kituo cha Afya Karatu kwa kujenga wodi ya wanawake na wanaume.

Alisema serikali pia imefanya upanuzi wa zahanati tano, kuongeza bajeti ya dawa kutoka Sh. milioni 131 hadi Sh. milioni 450 zilizokuwa zinatolewa kila mwaka. Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 7.4 kwa ajili ya kugharamia elimu bure, ujenzi wa madarasa 208, utengenezaji wa madawati zaidi ya 4,000, ujenzi wa nyumba za walimu 84, barabara ya changarawe kilomita 34 na kupeleka umeme katika vijiji 47 kati ya 57 vilivyokuwa havijaunganishwa na huduma hiyo.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili ijayo, serikali itahakikisha inavifikia vijiji 10 vilivyobaki kupata umeme wa uhakika.



Mgombea wa urais kupitia chama cha ADC, Queen Sendiga, akihutubia mkutano wa kampeni katika eneo la stendi ya maji ya chai, jijini Arusha juzi na kuahidi kujenga chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali ya Wilaya ya Arumeru (Patandi), endapo atachaguliwa kuwa Rais. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu alalama hujuma katika uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA Urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amelalamikia kile anachokiita hujuma kuelekea uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Jumatano ijayo.

Lissu, katika mkutano wake na waandishi wa habari jana mkoani Lindi, aliekeza lawama zake hizo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jeshi la Polisi na baadhi ya taasisi za umma, akidai zinamhujumu.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia tuhuma hizo, alidai ni uongo ambao anafikiri umeandaliwa kwa lengo la kuzusha taharuki kuelekea uchaguzi huo.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Lissu alisema tayari wataalamu wao wa chama wanazifanyia kazi hujuma zinazofanywa dhidi yake na taarifa itatoka kabla ya Jumatatu.

"Vitendo ambavyo tulivitabiri mwanzoni, tumeanza kuviona, tulisema hawawezi kushinda kwa huru na haki na tayari tumeona dalili hizo ama za kutaka kuharibu uchaguzi au kufanya wizi.

"Daftari la kudumu la mpigakura limetolewa siku chache zilizopita kila mahali katika nchi, kwa kuangalia haraka haraka na wataalamu wetu wanalifanyia uchunguzi wa kina na watatoa taarifa mapema, maeneo machache kunaelekea kuna mamilioni ya wapigakura hewa wameingizwa na vipo vituo hewa maelfu," alidai.

Mgombea huyo alisema ana ushahidi wa mwanzo unaoonyesha katika baadhi ya maeneo wameandika majina ya wasiokuwapo na wengine ni wanafunzi wadogo wasiokuwa na sifa na wanafundishwa namna ya kupiga kura.

"Hii ni dalili tosha wanafikiria wanaweza kuiba katika uchaguzi ambao hawawezi kuushinda, wanataka kufanya hivyo," alidai.

Lissu alidai wanataka kutumia vitendo vya kihalifu kubadilisha matokeo mahali ambako watu wameshindwa kutangaza wagombea wao kwa nguvu.

"Watu wetu ndani ya tume na wananchi wanatuambia wanachoweza kufanya ni kubadilisha matokeo katika vituo vya kupigia kura.

"Kutangaza wagombea kwa nguvu katika vituo vya majumuisho kuanzia ngazi ya kata, majimbo na tume, kutumia mabavu wanaotangazwa ndiyo wanakuwa washindi, tunapata taarifa nyingi kutoka vyanzo vyetu," alidai.

Lissu alitaja vitendo vingine ambavyo kwa sasa vinaongezeka ni matumizi ya vyombo vya dola na baadhi ya taasisi za umma kwa waziwazi ili kupunguza uwezo wao wa kufanya kampeni.

Alidai vitendo vingine ni kuzuiliwa kufanya kampeni, akirejea tukio la mkutano wake kupigwa mabomu ya machozi juzi mkoani Lindi.

**KAULI YA NEC**

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Charles, alisema tume ilishatoa ufafanuzi wa tuhuma kama hizo zilizotolewa na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, kwamba na wapigakura hewa wameandaliwa kwa lengo la kukibeba chama tawala katika uchaguzi huo.

"Jumatatu kama wanakuja na ripoti yao ya ufafanuzi, tusubiri hiyo Jumatatu aje na taarifa yake aje kuaibisha tume au aaibike mwenyewe.

"Hivi ni vitu vya kushangaza, mtu ajiulize 'mamilioni kweli au anataka kuleta taharuki?'. Tusubiri tuone kama NEC itaaibika maana ndilo wanalolitafuta," alisema.

**RATIBA YA KAMPENI**

Kuhusu ratiba yake ya lala salama, Lissu alisema wataendelea kama kawaida, leo akitarajiwa kufanya kampeni Ruvuma kisha Dodoma, Singida na baadaye Kilimanjaro na Tanga kabla ya kufunga kampeni Viwanja vya Kawe jijini Dar es Salaam Oktoba 27.

Alisema jaribio lolote la kutaka kuvuruga uchaguzi huo, litasababisha watu kupelekwa mahakama ya kimataifa ya kihalifu na tayari uchunguzi umeshaanza kwa matukio yaliyofanyika na ipo orodha ya watu wanaoangaliwa.

Lissu alitahadharisha kuwa yeyote akivuruga uchaguzi, ataingia kwenye orodha ya kwenda mahakama hiyo.

Alidai vyanzo vyao vya taarifa vimewaeleza kuwa siku tatu kuanzia leo kutakuwa na michezo michafu mingi dhidi ya viongozi, wanachama na wagombea wa upinzani.

Lissu aliwataka mawakala wao wahakikishe wanapata nakala za matokeo mapema ili wajue ushindi walioupata.

Lissu alisema tangu kampeni za uchaguzi mkuu zianze, CHADEMA ndiyo chama kilichofanya mikutano mingi kuliko vyama vingine vyote.

# RC aonya vijana vurugu uchaguzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewataka vijana mkoani hapa kuacha kurubuniwa na baadhi ya wanasiasa kufanya fujo wakati wa uchaguzi mkuu wa Jumatano.

Alitoa onyo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari mkoani hapa, zikiwa zimebaki siku tatu kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo.

Telack alisema kuna tetesi kuhusu baadhi ya vijana kutaka kufanya fujo siku hiyo ya uchaguzi mkuu, akiwataka waache kwa kuwa serikali imejipanga vyema kudhibiti viashiria vyote vya uvunjifu wa amani.

"Tarehe 28 mwezi huu ambayo ni siku ya Jumatano, tutakuwa na uchaguzi mkuu, hivyo nitoe tahadhari kwa vijana, wasirubunike kufanya fujo zozote zile, tutawashughulikia, tunataka uchaguzi umalizike kwa amani.

"Amani hii tuliyonayo nchini, mataifa mengi yanatamani ivurugike, na sisi hatutakubali, mtu ukishindwa, kubali matokeo, uchaguzi ni kama mpira, ukifungwa goli, jipange mchezo ujao," alisema.

Kiongozi huyo alisema wameshatoa maelekezo kwa wasimamizi wa uchaguzi kuwa watu wenye uhitaji maalum wakiwamo wazee, wajawazito na wenye watoto wadogo, wapewe kipaumbele kuanza kupiga kura na siyo kujipanga mstari.

Telack pia aliwaonya waandishi wa habari kuhusu kujihusisha na utangazaji wa matokeo kwenye vituo vya kupigia kura, akisisitiza kuwa kazi hiyo ni ya msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika.

Alisema waandishi wa habari hawapaswi kutangaza matokeo ambayo msimamizi hajayatangaza, ili wasilete taharuki.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo (kushoto), akimpa maelekezo Mwalimu Godfrey Matonya na mkewe, jijini Dodoma jana, baada ya kuwarejeshea Sh. million 22.4 walizodhulumiwa na kampuni ya Kabuguma, inayojihusisha na kukopesha matrekta ya kulimia. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# CHADEMA, ACT wafanya kampeni jukwaa moja

**Na Neema Hussein,** KATAVI

VYAMA vya ACT-Wazalendo na CHADEMA mkoani Katavi, vimeungana kufanya mikutano ya kampeni kwenye jukwaa moja, lengo likiwa kuhakikisha wanakin'goa madarakani Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Baada ya kumalizika kwa mkutano wa hadhara wa kampeni uliofanyika jana kwenye viwanja vya Maridadi Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Mgombea Ubunge wa Mpanda Mjini (ACT-Wazalendo), Stanslausi Kisesa, alisema toka wameungana, mwitikio wa watu ni mkubwa katika mikutano yao.

Alisema mbali na kuing'oa CCM madarakani, lengo lingine la ushirikiano wao huo ni kutatua kero za wananchi ambazo wabunge wa CCM wameshindwa kuzipatia ufumbuzi toka wakae madarakani kama vile ukosefu wa dawa hospitali na wanafunzi kukaa chini darasani.

"Kutokana na wito wa viongozi wa kitaifa, sisi wagombea wote tulikubaliana katika kikao kuwa tutashirikiana hasa pale tutakapoona kuna upungufu," alisema Kisesa.

Mgombea Ubunge, Rhoda Kunchela (CHADEMA), alisema akichaguliwa, atahakikisha anaondoa tozo wanazotozwa wakulima katika magazeti ambayo yaliwekwa na uongozi wa mkoa kuwadhibiti wanaposafirisha mazao yao.

"Yani leo ukikamatwa na magunia ya ufuta, ni afadhali ukamatwe na magunia ya bangi, kwanza haya masuala ya stakadhi ghalani yametoka wapi? Mbona mikoa mingine hamna yani? Mtu unapangiwa soko la kwenda kuuza mazao yako," alilalamika.

Alisema akishinda kuwa mbunge wa jimbo hilo, atashirikiana na madiwani kuhakikisha wanazitatua kwa pamoja zile kero ambazo hazijatatulika ikiwamo kuleta maji na umeme wa uhakika kwa wananchi wa Mpanda.

# CHADEMA yaahidi hospitali Ubungo

**Na Enock Charles**

MGOMBEA Ubunge wa Ubungo, Boniface Jacob, ameahidi kujenga Hospitali ya Wilaya ya Ubungo akipewa ridhaa ya kuliwakilisha bungeni, ili kusaidia kuboresha huduma za afya wilayani huko.

Katika mkutano wake wa kampeni Kata ya Kimara jijini Dar es Salaam juzi, Jacob alisema ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo uliokuwa unaendelea katika eneo la Kimara Baruti, ulisimama alipoondolewa katika nafasi ya Meya wa Manispaa ya Ubungo mwaka jana.

"Wananchi wa Ubungo mnajua 'figisu' nilizofanyiwa nikaondolewa katika nafasi ya meya, tangu wakati huo ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao msingi ulikuwa umeshawekwa umesimama," alisema.

Mgombea huyo alisema kwa sasa wananchi wa jimbo hilo wanatumia Kituo cha Afya Sinza kama hospitali na kiko mbali na maeneo mengine ya jimbo hilo, hivyo kuhatarisha maisha ya wagonjwa.

Alisema hakumalizia ngwe yake ya uongozi baada ya kufanyiwa kile alichokiita hujuma, lakini alijitahidi kutekeleza ahadi zake zote na kuwaahidi wananchi wa Ubungo kufanya kazi zaidi akichaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo.

Uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani umepangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, siku tatu zijazo.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeshatangaza kuwapo vituo vya kupigia kura 80,155, Watanzania 29,188,347 wenye sifa, wakitarajia kuchagua wabunge 390 na madiwani 5,350.

JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
Tarehe 23-10-2020

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU/JUMANNE tarehe 26-27/10-2020 kampuni ya **ALBION COMPANY LIMITED** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **HOLILI BORDER** kuelekea **MOSHI kupitia HIMO.**

2. Gari hizo zenye namba za usajili

**T 413 CZJ / T 830 AYH**
**UREFU 25 UPANA 5.4 KIMO 5.4**

**T 978 ATN / T 480 BLP**
**UREFU 25 UPANA 5.4 KIMO 5.4**

3. Gari hizo zinatoka **HOLILI BORDER** kuelekea **MOSHI** kupitia **HIMO.** Gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzaia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:30 jioni).

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115958902

RIPOTI MAALUM

# Unafahamu unywaji wa maji mengi unasababisha maradhi ya moyo?

## ■Madaktari bingwa wadokeza kilichojificha
## ■Janga liko zaidi kwa watendaji wa ofisini

**Na Mary Geofrey**

Ni imani inayotawala, ikiwamo kauli rasmi kutoka kwa wataalamu wa afya wanaopigia upatu tabia ya kunywa maji mengi, kwamba ni kinga dhidi ya baadhi ya maradhi, yakiwamo yanayohusiana na moyo.

Lakini, mtaalamu bingwa kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Profesa Mohamed Janabi, ana kidokezo kuhusiana na matumizi ya nadharia hiyo kiholela kwamba yanaweza kumrudisha mhusika katika maradhi zaidi.

Profesa Janabi, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo anasema maji hayo ya ziada yanakuwa na manufaa kwa mnywaji iwapo tu kuna kiwango sahihi cha kuushughulisha mwili wake hata maji hayo yakatumika kwa manufaa kiafya.

Kwa mujibu wa Profesa Janabi, katika hali ya kawaida, mwili wa binadamu huwa na kiwango cha wastani wa lita tano za maji zinazozokuwa kwenye mzunguko mwilini na panapotokea maji ya ziada pasipo kutumika, ni hali inayouchosha moyo na kuishia katika kuzalisha maradhi.

Mtaalamu huyo anafafanua kwamba mwili wa binadamu unapokosa shughuli ngumu zinazosababisha jasho kutoka, kiwango cha juu cha unywaji maji kinapaswa kisizidi kati ya lita moja na nusu hadi mbili kwa siku.

"Maji yanayohitajika kwenye mwili wa binadamu kwa siku ni lita moja na nusu, kama hamna joto wala hufanyi kazi ngumu, unasababisha hatari kwenye moyo wako.

"Mzunguko wa damu tayari una lita tano na wewe unakunywa lita tano, kwa hiyo unaulazimisha moyo kusukuma mara mbili zaidi na mwisho wa siku unajikuta una shida ya moyo," anatahadharisha.

Profesa Janabi anaeleza kwamba, wakati moyo wa mtu unafanya ya kusukuma maji ya ziada kuliko uwezo wake, athari inayofuata baada ya hapo ni baadhi ya chembe hai muhimu zinaanza kufa moja baada ya nyingine zikipishana na maradhi kuanza kuchukua nafasi yake.

Bingwa huyo wa maradhi ya moyo, alitoa katika hadhira ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani, Septemba 29 mwaka huu katika Viwanja vya Tanganyika Packers jijini Dar es Salaam.

Mtaalamu huyo anaelekeza kidole cha tahadhari hasa kwa watendaji wa maofisini na mazingira yanayofanana nayo kwamba mbali na hatari ya kuuchosha moyo, pia ziada ya maji hayo imebeba hatari kuyeyusha madini muhimu kwa mwili wa binadamu.




Profesa Mohamed Janabi,

### ULAJI NAO TATIZO

Profesa Janabi anataja sababu nyingine kubwa ambayo watu hawafahamu kama ni chanzo cha kuugua maradhi ya moyo kuwa ni ulaji usio wa mpangilio.

Anasema ulaji wa vyakula vya mafuta umekuwa ukitajwa na wengi kuwa tatizo kubwa katika kusababisha maradhi ya moyo, lakini siyo chanzo wala tatizo kubwa bali ulaji wa vyakula vya wanga ndiyo mzizi wa tatizo.

Anasema vyakula vya wanga kama ugali na wali vinavyoliwa mara nyingi na Watanzania huhatarisha usalama wa moyo na hivyo anashauri watu kupunguza ulaji wa aina hiyo ya vyakula.

"Ukiweza kujibana, basi unaweza kupunguza kula ugali na wali angalau ule mara mbili kwa wiki kwa vyakula hivi," anashauri Profesa Janabi.

Anasema ratiba ya vyakula hivyo pia ni lazima izingatiwe na walaji kwa usalama wa moyo.

"Mtu anakula saa tatu, nne hadi saa sita usiku sahani kubwa ya wali au ugali, akimaliza hapo anaingia kitandani analala, hapo badala ya chakula kufanya kazi kinaenda kukaa kwenye stoo," anatahadharisha Profesa Janabi.

Anasema mlundikano huo ndiyo husababisha zaidi madhara kwa mwili wa binadamu kama vile kutengeneza vitambi, shinikizo la damu na matatizo ya moyo.

Profesa Janabi anashauri kuwa muda sahihi wa kula chakula ni kuanzia saa 12 jioni hadi saa 1:00 usiku, ikiwa ni saa chache kabla ya kwenda kulala.

### HALI ILIVYO KITAIFA

Profesa Janabi anasema magonjwa ya moyo huchangia karibu asilimia 31 ya vifo vyote duniani na kwamba takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinabainisha kuwa kila mwaka, takribani watu milioni 18 hufariki dunia kutokana na maradhi hayo.

"Ni tatizo linaloonekana kuongezeka, takwimu zinaonyesha katika kila wanawake wanne na wanaume watano, mmoja anakabiliwa na tatizo la shinikizo la damu," anabainisha.

Anaongeza kuwa magonjwa ya moyo ni kati ya magonjwa yasiyoambukiza, ambayo kinga ni rahisi kuliko tiba, ndiyo maana WHO pamoja na Jumuiya ya Magonjwa ya Moyo Duniani baada ya kuona yanaongezeka, wakaamua kuanzisha Siku ya Moyo Duniani.

"Watu pia wanapaswa kuzingatia unywaji wa pombe kwa kiasi, kuacha uvutaji wa sigara, kula vyakula vinavyofaa, wazingatie kunywa dawa wanazoandikiwa (waliokutwa na matatizo haya) na wafanye mazoezi, wapunguze uzito uliopitiliza. Haya ni mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wa mtu bila gharama," anasema.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa JKCI tangu mwaka 2015 ilipoanzishwa hadi sasa, tayari imeshaona takribani wagonjwa 350,000 huku 6,000 kati yao wakifanyiwa upasuaji.

"JKCI tupo mstari wa mbele kutoa elimu ili watu waepuke magonjwa haya," anasema Profesa Janabi.

### BP IKO JIRANI

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa asilimia 70 ya wagonjwa wanaotibiwa JKCI, wanakabiliwa na tatizo la Shinikizo la Damu (BP).

Anasema takwimu zao zinaonyesha ndiyo tatizo linaloongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa katika taasisi hiyo tangu ilipoanzishwa rasmi mwaka 2015.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Samweli Rweyemamu, anasema wapo pia wengine wanaokabiliwa na tatizo la kuziba kwa mishipa ya damu inayosambaza damu kwenye moyo ambayo husababisha kifua kuuma.

"Kuna wengine wanaohitaji upasuaji na idadi inaongezeka kila siku. Kwa mfano, wale ambao mishipa ya damu inaziba, tunawazibua kwa upasuaji mkubwa au ule wa tundu dogo," anasema Dk. Rweyemamu.

Anabainisha kuwa hadi Desemba mwaka jana, waliwachunguza karibu wagonjwa 1,000, ambao awali walikuwa wakipewa rufani ya kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Daktari bingwa huyo anasema kuwa kwa siku, huwa wanaona wagonjwa kati ya 300 na 400, hali inayoonyesha kwamba watu wenye matatizo ya moyo wanaongezeka nchini.

Dk. Rweyemamu anatoa mfano kwamba Wilaya ya Temeke kwenye Viwanja vya Zakheem walipima watu 100 na kati yao, asilimia 18 walikuwa na BP na wengine moyo umetanuka. Pia, 21 walionekana wana matatizo ya moyo.

Anasema pia walifanya kazi kama hiyo katika viwanja vya Mwembe Yanga kwa watu 150 na kati yao, asilimia 22 walionekana kuwa na maradhi ya moyo. Anasema kati ya hiyo asilimia 22, asilimia 19 walikuwa na shinikizo la damu la juu.

Anaongeza kuwa idadi hiyo inawezekana kuwa ni ndogo lakini utafiti uliofanyika Dar es Salaam, unaonyesha karibu asilimia 30 wana shida ya shinikizo la damu.

"Sasa ukiwa na shinikizo la damu ni 'risk factor' (ishara hatari) ya kuziba kwa mishipa ya moyo hatimaye utafika kwetu tukuzibue kwa vifaa maalum," anasema Dk. Rweyemamu.

Anasema mtu akiwa na shinikizo la damu, moyo hutanuka na kuwa na dalili za kushindwa kufanya kazi, hivyo asilimia kubwa ya matatizo ya moyo kwa watu wazima yanaanza na presha.

Mratibu wa Tiba wa Manispaa ya Kinondoni kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Manispaa hiyo, Dk. Omary Mwangaza, anasema kipindi cha Julai na Agosti mwaka huu, katika vituo vya kutolea huduma za afya, waliibua wagonjwa wapya zaidi ya 600 wanaokabiliwa na magonjwa yasiyoambukiza.

"Shinikizo la damu na kisukari ni magonjwa yaliyokuwa yakiongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa, wagonjwa wote hawa tumewaingiza kwenye mfumo wetu wa matibabu," anabainisha.

# SUMA JKT yaokoa Mil. 400/- za ujenzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SUMA JKT imeokoa Sh. milioni 400 katika ujenzi wa kiwanda cha mabati na misumari jijini Dodoma kutokana na kuwatumia vijana na maofisa wake kujitolea kutekeleza mradi huo. Mradi wa ujenzi wa kiwanda unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni moja.

Wakati akikagua ujenzi wa kiwanda hicho juzi, Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema ujenzi wa kiwanda hicho umefikia asilimia 85.

Kanali Mabena alisema kiwanda hicho ambacho kinajengwa kupitia shirika lake la Suma JKT, kinatarajia kukamilika na kuanza kazi mapema mwakani. "Kiwanda kitasaidia kuwanufaisha wakazi wa Dodoma ikiwamo kutoa ajira kwa vijana," alisema Kanali Mabenona.

Alisema JKT imekuwa ikitoa gawio kwa serikali, hivyo kiwanda hicho kitachangia pia kuongeza pato la taifa na gawio kwa serikali ambalo jeshi limeshatoa kwa miaka mitatu mfululizo. Alisema jeshi hilo lina mpango wa kuanzisha viwanda vingine vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, akibainisha kuwa tayari wana kiwanda cha kuchakata mahindi cha Mlale, Songea na kile cha mpunga kilichoko Chita, Ifakara.

"Uchumi wa nchi umekua na kufikia uchumi wa kati. Kama jeshi, tunalo jukumu la kuhakikisha tunaunga jitihada za serikali ili kufikia uchumi wa juu zaidi," alisema Kanali Mabena. Aliwataka vijana hao kuzingatia maelekezo ya ujenzi ili mkataba ukiisha, wakafanye kazi kama hizo mitaani.

Mkuu wa mradi huo, Meja Erasto Tesha, alisema katika utekelezaji wa mradi huo, tayari wamepokea Sh. milioni 457.3 na kati yake, Sh. milioni 420.4 zimeshatumika.

Meja Tesha alisema kampuni wanayoitumia imeshasajiliwa, hivyo inafanya kazi kihalali katika shughuli za ujenzi zinazoendelea.

Alisema wanawashukuru vijana wanaojitolea katika ujenzi, akiwapongeza kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa katika ujenzi huo.

"Tunawashukuru sana vijana wanaojenga kwa sababu wanafanya kazi iliotukuka, hivyo wanastaili sifa," alipongeza Meja Tesha.

Aliwataka vijana hao kuwa makini na kazi wanazofanya maana zitawasaidia huko mbeleni.

# Baba na mtoto jela miaka mitatu kwa kumhonga DC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Dodoma, imewahukumu baba na mtoto kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. milioni 1.5, baada ya kukiri kutaka kutoa hongo ya Sh. milioni 1.2 kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi.

Washtakiwa hao ambao pia ni wafanyabiashara, Nahid Bahadur Hirji na mwanawe, Bahadur Abdallah Hirji, walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya kuahidi na kutoa rushwa kwa Katambi.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alibainisha kutolewa kwa hukumu hiyo alipozungumza na waandishi wa habari jana kuhusu kesi mbalimbali za rushwa mkoani humo.

Alisema kesi hiyo ya jinai namba 148/2019 ilitolewa hukumu Oktoba 19 mwaka huu na mahakama hiyo.

Alifafanua kuwa Julai mwaka jana, TAKUKURU iliwafikisha mahakamani huko wafanyabiashara hao baada ya uchunguzi kuonyesha walifanya jinai hiyo ya kumshawishi Katambi asichukue hatua stahiki dhidi yao kuhusiana na mgogoro wao wa kifamilia.

Alisema washtakiwa hao walihidi na kutoa kiasi hicho cha fedha kwa Katambi kinyume cha kifungu Na. 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Alisema pamoja na hukumu hiyo, mahakama pia imetaifisha Sh. milioni 1.2 zilizokamatwa wakati wa mtego wa hongo hiyo.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU imewarejeshea fedha kiasi cha Sh. milioni 28.97 wananchi wawili akiwamo mwalimu mstaafu, Stanley Matonya, ambaye kwa sasa ni mkulima katika Kijiji cha Itiso wilayani Chamwino.

Kibwengo alisema mwalimu huyo amerejeshewa Sh. milioni 22.4 alizodhulumiwa na Kampuni ya Kabugama ya jijini Dodoma Agosti 2016.

"Mstaafu huyo aliingia mkataba wa kuuziwa trekta moja aina ya Swarrag 744 lenye jembe moja pamoja na tela kwa makubaliano ya kulipa Sh. milioni 23.98 ambayo ni asilimia 50 ya thamani ya trekta.

"Pamoja na kulipa fedha hizo tangu Septemba 2016, mwalimu huyo hakupata trekta na alipofuatilia, aliambulia kurejeshewa Sh. milioni 1.5," alisema.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema kutokana na juhudi za mstaafu huyo kukwama, alitoa taarifa kwa taasisi hiyo na uchunguzi umewezesha kampuni hiyo kurejesha Sh. milioni 22.4 ambazo alikabidhiwa jana.

Alisema TAKUKURU pia imemrejeshea mkazi wa Jiji la Dodoma, Ahmed Talibu, Sh. milioni 6.49 ambazo ni malipo ya fidia ya kiwanja namba 214 Kitalu G eneo la Kikuyu South Extension jijini hapa kilichotwaliwa kwa ajili ya kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya mwendokasi.

"Mei mwaka huu, TAKUKURU ilipokea taarifa kutoka kwa Talibu kwamba ameshindwa kulipwa baada ya kuelezwa na Shirika la Reli (TRC) linaloratibu ujenzi huo kuwa tayari malipo ya fidia ya kiwanja cha mwanawe, Nasra Ahmed Talibu yalishafanywa kwa mwananchi mwingine," alisema.

Kibwengo alisema uchunguzi wa taasisi hiyo ulibaini fidia hiyo imelipwa kwa Noorjan Adulhamid Ahmed baada ya kuwasilisha nyaraka alizozipata kwa njia ya udanganyifu na kufanikiwa kumrejeshea fedha hizo jana Ahmed kwa niaba ya mwanawe.

Pia, alisema taasisi hiyo inaendelea kumtafuta mtuhumiwa aliyemuuzia kiwanja Noorjan na kumpatia nyaraka za kiwanja ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yake. Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya dhuluma ili hatua zaidi zichukuliwe dhidi ya watu wanaofanya hivyo.




Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Pwani na Dar es Salaam, Brigita Stephen, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa duka jipya la kisasa la kampuni hiyo, katika Mtaa wa Msimbazi, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 20 ya Vodacom nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DPP atangaza neema Songwe

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

OFISI ya Taifa ya Mashtaka imewahakikishia wananchi wa mkoani Songwe kutenda haki na kuwaondolea kero ya muda mrefu ya kutoshughulikiwa kwa mashauri yao kwa wakati kutokana na kukosekana kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mkoani hapa.

Katika hafla ya ufunguzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mkoani Songwe jana, Mkurugenzi wa Mashtaka, Biswalo Mganga, alisema:

"Yeyote atakayefanya fujo kipindi hiki ama kipindi chochote kile, atashughulikiwa, waache mara moja kwani serikali haiwezi kuwavumilia hao wote waliopanga kufanya fujo."

Mganga alisema tayari watu 24 Tunduma mkoani Songwe wametiwa mbaroni kutokana na kujihusisha na vurugu zilizosababisha mauaji ya kijana mmoja mpakani huko.

Mkurugenzi wa Mashtaka aliwahakikishia wananchi upatikanaji wa haki mkoani Songwe huku akisisitiza kuwa kutokana na mkoa huo kuwa mpakani, atahakikisha wanafungua ofisi nyingine mpakani Tunduma kwa lengo la kuzuia uhalifu wa kimpaka. Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangala, alimpongeza Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na ofisi yake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha haki na amani zinapatikana nchini. Alisema licha ya Mkoa wa Songwe kuwa mchanga, uhitaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ulikuwa mkubwa kutokana na mkoa huo kuwa mpakani na una mwingiliano mkubwa wa watu.

Alisema uwapo wa ofisi hiyo mkoani hapa, utarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wananchi juu ya ucheleweshaji wa upatikanaji wa haki.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Songwe, Kassim Mkwawa, alisema uwapo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mkoani Songwe, utarahasisha majadala ya kesi mbalimbali zinazohitaji uchunguzi, kushughulikiwa kwa haraka, akibainisha kuwa awali yalikuwa yakipelekwa Mbeya na kutumia muda mrefu kufanyiwa kazi.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Edson Makallo, aliwashukuru viongozi wa dini kwa namna wanavyoliombea taifa, akimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Songwe juu ya mtumishi yeyote wa serikali atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa, ofisi yake haitasita kutia saini barua ya kumsimamisha kazi.

Alisema watumishi kujihusisha na vitendo hivyo ni kukandamiza haki za watu wengine.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila Mtanzania anapaswa kulinda, kudumisha amani

**ILIKUWA** miezi, yakawa majuma na sasa zimebaki siku tatu kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa tano wa Rais, wabunge na madiwani tangu Tanzania ilipoingia katika mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Uchaguzi huo mkuu utafanyika kwa mara ya kwanza katikati ya wiki baada ya miaka mingi. Siku hiyo si nyingine bali ni Jumatano ijayo, Oktoba 28. Watanzania, wake kwa waume, wazee kwa vijana, wanatarajia kutumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi watakaoongoza katika nafasi tajwa kwa miaka mitano ijayo.

Watanzania hao, waliojiandikisha watatumia fursa hiyo kufanya uamuzi utakaotoa hatima ya uongozi wa nchi katika ngazi ya urais, ubunge na udiwani. Kwa maneno mengine, ndio walioshika mipini ya visu vyenye makali kwa ajili ya ama kuwaondoa madarakani walioko katika nafasi hizo au kuendelea kuwaweka kwenye viti hivyo.

Hatua hiyo ya wananchi walio na haki ya kufanya hivyo, itakuwa hitimisho baada ya kuwasikia wagombea na viongozi wa vyama husika wakijinadi majukwaani wakati wa kampeni kutoa sera na ahadi kemkem kupitia ilani zao za uchaguzi, zilizofanyika kwa takriban miezi miwili.

Katika kipindi chote hicho, wagombea hao wameeleza kwa kinagaubaga kuwa watafanya hiki na kile pindi wananchi watakapowachagua au kuendelea kuongoza dola au kuchukua sehemu zilizokaliwa na vyama vingine. Miongoni mwa ahadi ambazo zimechukua chati za juu ni barabara, umeme, afya na maji, vyote hivyo vikilenga kuwakomboa wananchi wanyonge.

Kwa mantiki hiyo, wananchi wataingia kwenye vyumba vya kupigia kura kwa lengo la kuwachagua wale wanaowaona wanafaa kuwa viongozi wao huku wakiwaamini kwamba ndio watakaosaidia kuondoa kero zinazowakabili pamoja na kuwatoa katika hatua moja kwenda nyingine yenye ubora zaidi.

Hakika ni muda mwafaka kwa yeyote aliyejiandikisha kutumia haki yake ya kidemokrasia. Kila mwananchi atakayekwenda kupiga kura, ni lazima atambue kwamba kura yake ina thamani kubwa katika ustawi wake, jamii na taifa kwa ujumla.

Kutokana na hali hiyo, mpigakura anapaswa kuhakikisha anafanya uamuzi wa kumchagua mtu bila kushawishiwa kwa ahadi za hapa na pale bali kwa kujua kuwa anampigia kura yule anayeona anafaa. Kinyume cha hapo itakuwa majuto kwake kwa miaka mitano ijayo.

Pamoja na ukweli huo, ni vyema Watanzania, bila kujali itikadi, imani, jinsia wala rangi, kutambua kwamba amani ni jambo la muhimu wakati huu na baada ya uchaguzi. Kwa maana hiyo, wanapaswa kuilinda amani ikiwa ni pamoja na kutojihusisha na vitendo vinavyoweza kusababisha tunu hiyo kuwa shakani.


Ili kuhakikisha amani inatawala, tunapaswa kufahamu kwamba siasa si uadui wala uhasama bali ni mfumo unaotaka watu wapambane kwa hoja zenye kujenga. Watu wanapaswa kupingana bila kupigana.

Kama ambavyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na ile ya Zanzibar (ZEC) zimekuwa zikisisitiza wananchi kufuata sheria na kanuni za uchaguzi, Watanzania wanatakiwa kutii maagizo hayo ili kuiweka nchi katika amani na utulivu hata baada ya uchaguzi.

Watanzania, hasa vijana, ni vyema wakatambua kwamba ustawi wa nchi uko mikononi mwao na njia pekee ni kujiepusha na ushawishi wowote unaoweza kuwaingiza katika ghasia ambazo zinahatarisha amani na maisha yao kwa ujumla.

Kila Mtanzania anayeitakia nchi amani, hana budi kuhakikisha anailinda kwa kila namna ili Tanzania iendelee kuwa na sifa ya kuitwa kisiwa cha amani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tahadhari za TMA, Wizara ya Afya zitutoe usingizini

Na Sabato Kasika

**WIKI** ya pili ya mwezi ujao, mvua kubwa inatarajiwa kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo ya Morogoro, Njombe, Mbeya, Iringa, Songwe, Lindi, Mtwara, Dodoma, Ruvuma na Singida.

Hii ni kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ambayo inasema mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kusini.

TMA inataja maeneo mengine kuwa ni Kanda ya Kati pamoja na Pwani ya Kusini na kutaka maeneo yaliyotajwa, kuanza kuchukua tahadhari ili kukabiliana na athari zitakazojitokeza.

Tahadhari hiyo inatolewa huku kukiwa na nyingine iliyotolewa wiki iliyopita na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kuwataka wananchi kuzingatia kanuni za afya kutokana na mvua. Wizara hiyo inasema kuna uwezekano wa kuibua magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara damu na yanayoenezwa na mbu kama vile malaria na dengue, iwapo tahadhari hazitachukuliwa.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, anazitaja baadhi ya kanuni zinazotakiwa kuchukuliwa kuwa ni kuchemsha maji ya kunywa, kuepuka kula chakula kilichopoa ama kuandaliwa katika mazingira yasiyo safi na salama.

Kanuni nyingine ni kutumia ipasavyo, vyoo na kunawa mikono kwa maji safi na tiririka na sabuni kabla ya kula, baada ya kutoka chooni, baada ya kumnawisha mtoto aliyejisaidia na baada ya kumhudumia mgonjwa.

Aidha, wananchi hawatakiwi kutotapisha vyoo na pia kujikinga kuumwa na mbu kwa kutumia vyandarua, kusimamia usafi katika mifumo ya majisafi, majitaka na mitaro.

Nikirejea kwenye hoja yangu, ni kwamba majanga ya asili kama mvua yanaweza kuleta madhara ambayo wakati mwingine yako juu ya uwezo wa jamii, hivyo kuchukua tahadhari ni jambo la muhimu.

Kwa mfano kutotiririsha maji taka wakati wa mvua ama kuzingatia suala la usafi kwa ujumla, yote hayo yako ndani ya uwezo wa jamii, kinachotakiwa ni kuchukua hatua kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.

Mafuriko yatokanayo na mvua, ni miongoni mwa majanga ya asili, ambayo yamekuwa yakiikumba baadhi ya mikoa nchini na kusababisha madhara yakiwamo watu kupoteza maisha na mali.

Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa, ambayo hukumbwa na janga hilo hasa maeneo, ambayo hayajapimwa, na kusababisha watu hukimbia kutokana na nyumba zao kujaa maji na kwenda kujihifadhi kwingine hadi hali inapotulia.

Zinaponyesha mvua kubwa, wakati mwingine baadhi ya barabara nazo hujaa maji na kusababisha magari kushindwa kupita, na hivyo kuletwa mitumbwi ya dharura kuvusha watu. Ni kweli kwamba, majanga ya asili hayaepukiki, lakini suala la kila mmoja kuchukua tahadhari ni la msingi, hasa kufuata maelekezo yanayotolewa na mamlaka husika, kwa ajili ya usalama.

Watu wanaoishia mabondeni watakuwa ni mashahidi, kwamba walishapewa tahadhari za muda mrefu wakitakiwa kuhama maeneo hayo kwenda kwingine, kwa kuwa huko waliko si sehemu salama kwao. Si wote ambao wanaendelea kuishi huko bali wapo ambao walishaitikia wito wa mamlaka husika na kuhama lakini wengine bado wanaendelea kuishi maeneo hayo hatarishi.

Matokeo yake ni kwamba, kila mvua inaponyesha, nyumba zao hujaa maji yenye taka mbalimbali vikiwamo vinyesi vya binadamu na hivyo kulazimika kuyahama makazi yao kwa muda.

Kwa hali kama hiyo, ni wazi kwamba watakiwa kuhama jumla na kwenda kwingine kwa sababu katika mazingira hayo, afya zao zinakuwa hatarini wana nafasi ya kulinda afya zao. Ni vyema kutambua kuwa majanga ya asili hayaepukiki, lakini kuchukua tahadhari ni suala la muhimu ili kuwa salama zaidi kuliko kuendelea kung'ang'ania kwenye mazingira hatarishi.

Nikumbushe tu kwamba utabiri wa hali ya hewa ni mojawapo wa nyenzo muhimu zinazoweza kuokoa maisha na pia kuepusha madhara makubwa yatokanayo na uharibifu wa miundombinu baada ya mvua na mafuriko.

Mamlaka ya Hali ya Hewa imekuwa ikijitahidi kutoa tahadhari kwa watu wanaoishi maeneo ambayo si salama, lakini unaweza kusikia baadhi yao wakidai kwamba, kama ni mafuriko yatapita na wataendelea kuishi.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA

# Somo toka upinzani kuwa/kutokuwa umoja



Nkwazi Mhango, Canada

WIKI mbili zilizopita, safu hii iliangazia namna wapiga kura watakavyochagua kwa kuzingatia baadhi ya mambo. Wiki hii tunawaangazia wachaguliwa tukigusia udhaifu na ubora wa baadhi ya uamuzi wao. Hapa tutaangalia procedure zaidi ya sera. Pamoja na ugumu na umuhimu wake, uchaguzi wa mwaka huu ni rahisi kutabiri ni mambo gani yatakuwa turufu kimkakati kuliko chaguzi nyingine zilizopita.

Leo, tutaangalia kwanini ni rahisi kunusa hali itakuwaje na sababu za kufanya hivyo.

Pamoja na ukweli kuwa kushinda na kushindwa ni matukio tegemewa na ya kawaida, nani atashinda au kushindwa siyo. Kufikia hitimisho wakati wa kuelekea kwenye kilele cha zoezi hili adhimu huhitaji ujuzi wa kuangalia viashiria wezeshi.

Kwa kuzingatia sayansi hii, safu hii, leo, itaonyesha vitu vitakavyoamua ushindi.

Mshindi atakuwa mmoja na watakoshindwa ni wengi. Hili halina utata. Kwa kuzingatia ukweli huu, zifuatazo ni sababu zinazonishawishi kusema bila hofu wala woga kuwa vifuatavyo ni vigezo ambayo wagombea wanapaswa kuviangalia kwa makini ili kushinda.

Ieleweke kuwa hatulengi kupendelea au kuonea chama au kambi yoyote.

Yafuatayo ni matokeo ya sayansi ya uchambuzi wa masuala ya kijamii na kisiasa inayoweza kufanywa na yeyote mwenye utaalamu katika fani hii.

Leo tutatoa faida zaidi kwa upinzani si kwa vile tuna ugomvi na wapinzani wao.

La hasha. Ni kwa vile tuna marejeo ya chaguzi mbalimbali zilizopita nchini nje ya nchi.

Mosi, bila upinzani kuungana na kuja na mgombea mmoja, kuna uwezekano hili likaathiri vibaya fursa ambayo washindani wao hawataichezea.

Hii ni kutokana ukweli kuwa umoja ni nguvu na utegano ni udhaifu. Hii halina mjadala. Hivyo, upinzani ungeliangalia hili kwa makini na kulishughulikia kabla ya siku ya kupiga kura.

Siku zote, vita ya panzi ni neema ya kunguru. Kuwa na nguvu ya pamoja hakuna mjadala. Tofauti na uchaguzi wa mwaka 2015, upinzani ulisimamisha mgombea mmoja chini ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) kipindi hiki, vyama vyenye ushawishi vimekuja kila mmoja na mgombea wa vyake.

Huu ni udhaifu mkubwa ambao ni mtaji mkubwa kwa wapinzani wake.

Ukiwa na washidani waliogawanyika, unashinda kirahisi. Hili halina ubishi hata kidogo.

Kwanini upinzani hautaki kuona hatari ya utengano huu. Kama kila mtu angesimamisha mtu wake mwaka 2015, mgombea wa UKAWA asingeweza kufanya vizuri kama alivyofanya tena ndani ya muda mfupi alipata zaidi ya asilimia 40 kutokana na muungano wa upinzani ambao kwa sasa haupo. Je, hili nalo upinzani utamlaumu nani? Kwanini wana mikakati wa upinzani wameshindwa kuona jambo rahisi kama hili? Kama upinzani utaungana, utawapa wapinzani wao kibarua cha ziada cha kupambana na hoja za pamoja badala ya sasa ambapo hata hoja zao zikipuuzwa hakuna madhara yatakayoonekana wazi wazi.

Pili, upinzani kwa sasa una kazi ngumu kuibua sera mbadala za pamoja zingetosha kujibu zile za wapinzani wao. Hili nalo linahitaji umoja.

Tutatoa mfano mmoja wa Afrika na dunia. Nchi nyingi za magharibi zimekuwa zikinyonya nchi za kiafrika kwa kufanya biashara na nchi moja moja badala ya pamoja. Zinatumia ukosefu wa umoja wa Afrika kuendelea kuinyonya.

Tatu, ukiachia mbali ukosefu wa umoja, upinzani una kikwazo kingine kikubwa yaani kuosefu wa uzoefu ikilinganishwa na ule wapinzani wao ambao watatumia uzoefu wao kuwahenyesha kirahisi kwa kupiga pale walipogawanyika, pale utengano wao utakaposababisha waanze kugombea kushinda kura kwenye majimbo mbalimbali ambapo wangeweka mgombea mmoja wa upinzani.

Kimsingi, hata kama udhaifu siku zote umekuwa dhaifu, huu mgawanyiko utaudhoofisha zaidi kiasi cha kutofua dafu mbele ya adui aliyeshikamana kuliko wakati wowote wa maisha yake ya miaka ya karibuni.

Nne mbali na sababu tajwa hapo juu, kutokuungana kwa wapinzani hata kwa ajili ya uchaguzi tu, kunatoa nafasi kwa washindani wao kuwapa hali ngumu tokana na kuwa na mtandao mkubwa na mpana nchi nzima, ambao wapinzani hawana kama hawataungana.

Hii ni mbali na kuwa na wanachama na wapiga kura wengi. Kuwa na matandao mkubwa ni jambo moja na kuufikia ni jambo jingine ukiachia mbali kuutumia. Wapinzani wangeungana na kugawana majimbo, nina hakika wangekuwa na mtandao mpana nchi nzima na kuweza kuepuka ughali wa kusimamisha kila chama mtu wake.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania mjue utamaduni unatufariki!



Na Joseph Kulangwa

KWA wale mliozaliwa mijini, hamtanibishia nikiwaambieni kuwa wakati mnazaliwa na kupata fahamu na kutambua hiki na kile, mlijikuta mkiwasiliana na wazazi wenu kwa Kiswahili. Anayebisha na anyooshe kidole nimuumbue mbele ya wazazi wake.

Na mpaka sasa baadhi yenu pamoja na kubalehe na kuvunja nyungo, hamjui hata lugha za baba na mama zenu, mnazungumza Kiswahili na kuokoteza neno moja moja la kilugha kutoka kwa wazazi hao. Sana sana wengi wenu mtajua kusalimia na kunyamaza na hata mkijibiwa hamwezi kurudishia. Nani anabisha?

Lakini pamoja na yote hayo hamjahoji kwa nini hamwelewi lugha za baba na mama zenu wa kuwazaa. Na wala hamshangai kwa nini. Ni kwa sababu mnapata kila mnachokitaka kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hamwoni tena umuhimu wa kujifunza lugha za jadi, kwa sababu mnaona hazikusaidieni.

Mnaona kabisa, kwamba Kiswahili kinakuunganisheni na jirani zetu, kinakuunganisheni shuleni, kinakuunganisheni vyuoni, makazini na hata vijiweni. Kama ndivyo sasa Kijita cha nini? Kihaya cha nini? Kisubi cha nini? Kisukuma cha kazi gani? Kizaramo kinakusaidieni nini?

Wanaotaka kujielimisha ndio wataanza kuuliza kwa nini hatuzungumzi kikwetu na badala yake tunazungumza Kiswahili 24/7? Wanaotaka kuelimisha watajibu kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha iliyotuunganisha Watanganyika, na hatimaye Watanzania, wakati tunadai Uhuru. Kiswahili ndicho kinatufanya tudai haki zetu hata sasa.

Wafafanuzi watakwambia Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere (PKA) na wenzake, walitumia lugha hiyo adhimu kutuunganisha katika kudai uhuru wa kujitawala, na hatimaye tukafanikiwa na hivyo kuendelea kukitumia kujiletea maendeleo tuliyonayo sasa na tunayoendelea kuyasaka.

Kwa muktadha huo huo, ndiyo sababu tunaupenda utamaduni wetu na kujivunia. Tutajiuliza utamaduni upi sasa? Wa makabila yetu au wa Kiswahili? Utajibiwa ni wa Kiswahili uliotokana na mchanganyiko wa makabila yetu. Je, ni kweli utamaduni wetu tunao na ni upi? Unajitanabahisha vipi? Kwa nyimbo, ngoma, mashairi, mavazi, chakula, muziki, mitindo? Jibu ni vyote.

Lakini wadadisi wakikaa chini na kuchunguza hicho tunachikiita utamaduni wetu, wanabaki na maswali mengi na wanapokosa majibu wanabaki kuduwaa. Tunaimba nyimbo gani sasa? Tunacheza ngoma zipi? Tuna mashairi yapi, kwani kuna waghani wangapi waliopo? Tunavaaje? Chakule chetu je ni kile? Wana mitindo wetu je, ni wa kitamaduni? Hapana! Ndilo jibu.

Zamani tulisikia nyimbo redioni, majukwaani na kwingineko zikihimiza Utanzania, kina Mzee Mwinamila, kina Mzee Makongoro wa Hiari ya Moyo? Ngoma za kina Nyunyusa ambazo sasa tunaona zinafanyiwa 'remix', mashairi yako wapi redioni? Hahahaaa, tunavaa kata-kei na vimini, tunakula chipsi na baga, tunacheza Bongofleva, mitindo ya Ughaibuni! Watanzania hao!

Miaka fulani hivi, tukaibuka usingizini na kuhanikiza kuja na vazi la Taifa. He! Tukaishia kukatakata Bendera ya Taifa na kujibandika viraka kwenye Kaunda Suti! Wengine wakabandika mifuko ya Bendera ya Taifa, wengine ukosi wa Bendera hiyo nakadhalika.

Enzi hizo tukipokea wageni wetu wa kitaifa kwa ngoma na nyimbo zetu za Kitanzania, zilizojaa maadili ya Mtanzania, zikionesha umoja, ushirikiano, ukarimu na amani ya nchi yetu kwa wageni. Nyimbo na ngoma za staha zaidi zilioneshwa.

Juzikati hapa nikashangaa mgeni wa kitaifa akipokewa kwa wimbo wa Bongofleva unaitwa Uno. Baadhi ya maneno yake yaliyosikika na yanayosikika hadi leo, ni eti "Uno linawaokoa makahaba..." Jamani, mgeni wetu kweli wa kitaifa, anaimbiwa wimbo huo na mwimbaji anakatika viuno mbele yake!!

Tukae tena tujiulize tunakosea wapi? Hatuna nyimbo za maana? Hatuna midundo na mikong'osio ya utamaduni wa Mtanzania kweli? Hivi ni lazima tuige midundo ya kigeni na kuingiza Kiswahili na kutamba eti tunatangaza utamaduni duniani? Tutafiti.

Kwa nini tulitelekeza Achimenengule ya John Komba (PKA)? Tuijenge Singeli basi, naona inanukia Kitanzania zaidi, mnaonaje wananzengo wenzangu? Alamsiki.

## KONA YA UKWELI

# Wagombea msiwe chanzo cha vurugu kwa kuyakataa matokeo



Na Thobias Mwanakatwe

OKTOBA 28, mwaka huu, Watanzania watashiriki kupiga kura kuchagua rais, wabunge na madiwani.

Mchakato huo wa upigaji kura unafanyika baada ya kumalizika kwa kampeni siku moja kabla ambapo wananchi walipata fursa ya kusikiliza sera na ilani za wagombea wa vyama zaidi ya 15 vinavyoshiriki uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Ni matumaini yangu kwamba kila mwananchi alipata fursa ya kuwasikiliza wagombea wote, hivyo bila shaka atafanya uamuzi sahihi kwa kumchagua kiongozi atakayewaletea maendeleo.

Uchaguzi wa mwaka huu naweza kusema umekuwa tofauti na mwingine wowote ulipita kwani safari hii tumeshuhudia baadhi ya wagombea wamekuwa wakizungumzia vurugu, shari na uchochezi badala ya sera.

Lakini wakati kampeni zikaendelea kukawa na minong'ono kwamba baadhi ya wagombea wanaotoa maneno yenye kuhatarisha uvunjifu wa amani wametumwa na wafadhili wao wa nje.

Binafsi, baada ya kusikiliza minong'ono hiyo, nikajiuliza hivi mfano ikitokea vurugu hao wanaohubiri mambo hayo wao pamoja na familia zao, ndugu zao, jamaa zao wakati huo watakuwa wapi?

Watanzania wenzangu, niwakumbushe kuwa amani ya nchi ndio msingi wa kila kitu, hivyo wanasiasa wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu wanapaswa kufahamu hilo na kama msingi wa kulinda utaifa, wanapaswa kusisitiza amani na kuwa tayari kuilinda kwa gharama yeyote.

Lazima tukumbuke kuwa Tanzania kwa miaka mingi tangu tupate uhuru imekuwa nchi yenye kupigiwa mfano kwa kuwa na amani na utulivu wa watu wake.

Naamini kila Mtanzania analo jukumu kubwa la kulinda amani ya nchi bila kujali nafasi yake na wanasiasa wana dhamana kubwa zaidi kutokana na ukweli kuwa baadhi yao wamekuwa wakitoa maneno ya yenye kuhatarisha amani na utulivu wa nchi.

Jambo lingine ambalo limejitokeza na ambalo linaweza kuwa chanzo cha kutokea kwa vurugu ni kauli za baadhi ya kugombea kuanza kusema kwamba hawatayakubali matokeo ya uchaguzi.

Mfano, wagombea urais wa vyama viwili vikubwa vya upinzani wakihojiwa kwa nyakati tofauti na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) wametoa masharti ya kukubali matokeo ya uchaguzi.

Kama tunavyofahamu, jukumu la kutangaza matokeo ya uchaguzi ni la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kule Zanzibar ni Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Ninachojiuliza kama wagombea wao wameshaanza kuonyesha dalili za kukataa matokeo wanataka nini kama si kutaka kusababisha vurugu na uvunjifu wa amani.

Wagombea hao wanajenga hoja kwamba watayakataa matokeo ya uchaguzi kwa kigezo kwamba uchaguzi si huru na wa haki. Mimi najiuliza hao wagombea kwa nini kama walijua kuwa uchaguzi hutakuwa huru na wa haki waliamua kuingia kwenye kinyang'anyiro.

Nadhani wagombea hawa wanataka kuwachochea wafuasi wake wajiingize kwenye vurugu kwa kuwaaminisha kwamba uchaguzi haukuwa huru na wa haki.

Lakini pia mgombea unapoanza kutia shaka na uchaguzi na kwamba utayakataa matokeo ni dalili kwamba wewe umeshakubali kushindwa hata kabla hujapigiwa kura kwa hiyo unatafuta huruma ya wananchi wakuunge mkono kwa kisingizo kwamba uchaguzi usio huru na wa haki.

Kama wagombea hao wanataka kutumia vurugu ili kufikisha ujumbe kwa wafadhili wao sisi Watanzania hatutakubali, nchi yetu haijazowea vurugu, waasisi wetu wa taifa hili walitulea katika maadili kudumisha amani na utulivu.

Nampongea Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk. Willibrod Slaa, amewaka wazi kuwa jumuiya za kimataifa kimsingi haina mamlaka ya kuingilia nchi katika mambo yake kwa sababu kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mikataba ya Umoja wa Mataifa ambayo inaheshimu mambo ya ndani ya nchi.

Viongozi wenye kuhubiri na kuiombea nchi yetu iingie kwenye machafuko na kuleta mgawanyiko miongoni mwa Watanzania hawana nafasi na wananchi wanapaswa kuwakemea na kuwakataa.

Nasema hivyo kwa sababu Tanzania inahitaji amani kwa ajili ya ustawi wa taifa na hasa wakati huu ambao nchi inapiga hatua kubwa za kimaendeleo chini ya usimamizi wa serikali ya awamu ya tano hatua ambazo zimelifanya taifa liwe mfano wa kuigwa na mataifa mengine duniani.

**Kwa maoni na ushari; Email- mwanakatwe2015@gmail.com**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**
**MUNGU UBARIKI UCHAGUZI**

## DARASA LA NDOA

# Umuhimu wa kutambua haiba kuimarisha uhusiano wa ndoa - 3



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

KATIKA kuna watu wenye sifa na haiba tofauti. Miongoni mwa haiba hizo ni Koleriki (Choleric). Neno choler ni neno lenye maana ya -enye hasira. Koleriki ni watu wenye hisia zilizojificha.

Kwa kawaida, koleriki huogopa kujiingiza katika uhusiano na mtu kwa kuwa si wavumilivu, wanapenda kujitegemea. Hali hii ya kutovumilia, inawafanya wakati mwingine kujitenga na uhusiano. Wako Koleriki walioamua kutokuingia katika uhusiano kabisa kwa kuhofia bughudha za kiuhusiano.

Ikiwa mwenzi wa Koleriki hana busara pale unapotokea ugomvi, kuna uwezekano wakaachana kwani tabia yao inaambatana na misimamo mikali waliyonayo. Pia ni wagumu kusema samahani. Vile vile hujikuta wanatoa maneno mabaya.

Wakati mwingine, watu wa jinsi hii wanapokosea husingizia vyanzo vya makosa hayo watu wengine. Hawakubaliani na uhalisia. Watu wa jinsi hii, huweza kuwa na uamuzi wa haraka kiasi cha kutoonesha uvumilivu endapo mwenzi amekosea.

Sifa zingine za Koleriki ni wazungumzaji kiasi fulani, lakini ni watu wenye hasira za haraka sana. Hata hivyo, hawadumu na hasira kwa muda mrefu kwa sababu ya kupenda kuzungumza. Watu katika kundi hili wanapenda kuonekana, kusifiwa na kutambulika. Ni wepesi wa kutenda mambo, kujifunza na kuanzisha ufahamu au mambo mpya.

Wana ujasiri na ni watu wenye uwezo wa kufikiri na kufanya uamuzi na kutekeleza kwa gharama yoyote, kwani huwa hawataki mchezo wawapo kazini, hawapendi mambo yaharibike mikononi mwao.

Koleriki ni wakosoaji wazuri, kupinga mambo hadharani au waziwazi; ni wakosoaji sana hata kwenye suala la tendo la ndoa. Ni watu wa mabavu; ni wapambanaji; kama ni mwanamke, hupenda kuwaongoza waume zao. Huamini katika mafanikio na wanapenda kazi kupindukia. Ni wakatili wakikosewa. Kama ni mwanamke, huwa na maneno makali na wakati mwingine huonekana ni mjeuri na si mtiifu.

Koleriki ni watu makini sana na hawapendi kufuatilia mambo madogo madogo, hasa yasiyowahusu. Hawapendi kuona watu wengine wakionewa; wanajipenda na kujisikia sana; wenye kejeli na wanaweza kutoa matamko yenye kuumiza wengine, hivyo, hawana marafiki wengi.

Ni wenye hisia sana, yaani, ama ni wakali sana au wenye huruma sana, na wanaweza kukasirika sana na kupayuka. Si wapole, bali wakali; si wazuri katika kuonyesha upendo na mapenzi. Ni watu wenye chuki sana na vinyongo.

Koleriki hawajali sana wenzi wao, kwani wanapenda sana kazi kuliko familia; Si wavumilivu hasa wanapokosewa. Huonekana wajuaji kwa kuwa wanafahamu vitu vingi, hivyo, kutokupendwa sana na watu wengine. Ni wagumu kuomba msamaha; hawatikiswi na misukosuko ya kile wengine wanachofikiri. Si wepesi wa kukata tamaa hasa wanaume. Hupendelea kuwa kivyao kutimiza matakwa yao. Uhusiano unapokuwa mgumu hupata sana msongo wa mawazo.

Hawa ni watu wenye msimamo mkali usioyumbishwa kirahisi. Si wepesi kushawishika kwa mambo mapya. Ni watu wanaopenda kusifiwa kwa kazi walizofanya na si kwa maneno wanayosema. Ni watu wanaopenda kujitegemea, kwa sababu hiyo, hawapendi kuombwa misaada. Na hata akitoa msaada ni kwa sababu ya kutaka watu wasije kusema hana fedha.

Koleriki hawapendi kupingwa. Kwa hiyo, hutaka watu wote wakubaliane naye hata kama hawajaridhika. Ndio maana wengi wao huwa watu wa uongozi wa kimla. Ni watu wasiojua kuonesha hisia za upendo. Ni wakavu sana katika masuala ya mapenzi ndiyo maana wengi huchelewa sana kupata wenzi kwa sababu huogopwa kuwa hawajui mapenzi. Hivyo, ukioa au kuolewa na Koleriki, usitarajie neno "I love you" na ukimwuliza kwa nini, atakuambia, si niliishakuambia siku ile ya ndoa.

Hata hivyo, Koleriki wa kiume anapomwoa Melankoli (wa Kike) wataendana sana, kwa sababu Koleriki anapopanda juu akiudhiwa, basi inakuwa rahisi kwa Melankoli kushuka kutokana na haiba zao.

Wanasaikolojia wanashauri kuwa Koleriki asimwoe/asiolewe na Koleriki mwenzie. Ndoa zao mara nyingi hazidumu, waswahili husema, "mafahari wawili hawakai zizi moja". Kwa ujumla, sayansi ya tabia inasema kuwa, kundi linaloweza kuishi na kuoana wenyewe kwa wenyewe bila changamoto sana ni Flegmatiki tu.

Swali la msingi ambalo mtu anaweza kujiuliza ni hili: Je, mtu anaweza kuwa na sifa zaidi ya moja kutoka katika makundi haya manne ya haiba, yaani Melankoli, Flegmatiki, Sanguine au Koleriki? Jibu ni ndio. Mtu anaweza kuwa na mchanganyiko wa sifa zaidi ya moja.

Hii ndiyo kusema kuwa, mtu anaweza kuwa na sifa za Melankoli na kwa sehemu akawa na sifa za Flegmatiki au Sanguine au Koleriki. Hata hivyo, lazima awe na sifa za pekee ambazo ndizo zitakazomtambulisha zaidi kuliko zingine kwamba yeye ni mtu wa aina gani.

■ **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya Tanzania Marriage and Child Care (TaMCare) inayojihusisha na masuala la ndoa na malezi ya familia. Anapatikana kwa barua pepe: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

OKTOBA 25, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili






Ukurasa 14

**Jinsi ya kutengeneza tomato sauce**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Bustani hupendezesha nyumba ikipangiliwa vizuri



## HARUSI

Ukurasa 12



## 'DREAD LOCKS'

# Nywele zinazoleta umaridadi

Ukurasa 14

# Mweleze mtoto kwa nini unamchapa

**Na Moses Ismail**

NI jambo la lazima kwa kila mzazi, kumuadhibu mtoto wake pale anapofanya jambo la ovyo, lenye kukera na lililo nje ya misingi ya maadili.

Mara nyingi wazazi wengi hutumia adhabu kuchapa, kufinya, kumrusha kichura au mazoezi mengine ya aina hiyo, na wengine wameenda mbali zaidi.

Walioenda mbali zaidi ni wale waliofikia hatua ya kuwajeruhi watoto wao ama kwa moto, kwa vitu vyenye ncha kali au hata kuwanyima chakula kwa muda mrefu kiasi mpaka majirani wanaingilia kati kumuokoa mtoto.

Kwa sisi Waafrika, kumuadhibu mtoto ni sehemu ya malezi mema na kunakubalika ingawa pia kuna aina fulani ya adhabu hazikubaliki hasa zile zinazoleta majeraha ya mwili kwa mtoto.

Lakini, kwa nini mzazi anachukua hatua ya kumuadhibu mtoto wake pale anapokosea? Iwe kumchapa kidogo, kumchapa sana, kumnyima chakula au kumchoma moto au aina yoyote ile, kwa nini mzazi anafanya hivyo?

Unapowauliza wazazi au walezi swali hilo, kama nilivyofanya, wengi wao watakujibu jibu unalolitegemea, kuwa wanamrekebisha mtoto na kumjenga katika maadili mema ingawa wengi pia wanapinga adhabu za kujeruhi.



"Mtoto anapokengeuka, lazima atandikwe kidogo, akemewe na hata ikibidi unaweza kumnyima mlo mmoja ili ajirekebishe. Ukimwacha (kwa kuogopa asilie) utakuja kulia wewe." Anasema Bakari Ussi, mkazi wa Ununio, Dar es Salaam.

Lakini, ni kweli kumuadhibu mtoto kwa kumpiga, kumrusha kichura, kumnyima chakula, kumchoma moto au aina nyingine za adhabu kama kumfokea kunasaidia kumrudisha mtoto kwenye maadili mema?

Hapana, hakusaidii. Adhabu yoyote ile, hata iwe kumpa mtu pilau na soda. inalenga kumuumiza mtu kihisia na kimwili, kwa maana hiyo ina madhara ama ya kiakili au kimwili. Kwa hiyo adhabu si kitu kizuri.

Kwa hiyo unapomuadhibu mtoto unatimiza lengo la adhabu, unamuumiza kiakili au kimwili. Na katika hali kama hiyo, lengo la kumrekebisha linaweza lisitimie na badala yake unaweza kumjenea kiburi ama usugu au akuchukie mzazi.

Lakini mzazi pia anaweza kumchapa mtoto, kumnyima chakula au vitu vizuri lakini bila ya kumuumiza kihisia. Njia hii ni ile ya kumweleza kwa nini unamchapa au unamnyima unachomnyima.

Mtoto anapaswa kuambiwa kosa lake kwa upole ili ajirekebishe. Ikibidi kuadhibiwa inapaswa aelezwe ni kwa nini anaadhibiwa na nini madhara ya kosa lake, hii itasaidia kumfanya ajue ubaya wa kosa lake na kujirekebisha."

## NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Majibu wiki iliyopita**

**Le quiz du week - end**

1. Kitenzi "Être" katika "Subjonctif" hunyumbuliwaje katika nyakati zilizowekwa hapo chini?

**Subjonctif**

Présent

| | |
|---|---|
| Que je | sois |
| Que tu | sois |
| Qu'il/elle | soit |
| Que nous | soyons |
| Que vous | soyez |
| Qu'ils/elles | soient |

**Imparfait**

| | |
|---|---|
| Que je | fusse |
| Que tu | fusses |
| Qu'il/elle | fût |
| Que nous | fussions |
| Que vous | fussiez |
| Qu'ils/elles | fussent |

**Passé**

| | | | |
|---|---|---|---|
| que | j' | aie | été |
| que | tu | aies | été |
| qu' | il/elle | ait | été |
| que | nous | ayons | été |
| que | vous | ayez | été |
| qu' | ils/elles | aient | été |

**Plus - que - parfait**

| | | | |
|---|---|---|---|
| que | j' | eusse | été |
| que | tu | eusses | été |
| que | il/elle | eût | été |
| que | nous | eussions | été |
| que | vous | eussiez | été |
| qu' | ils/elles | eussent | été |

**NB:** Katika "subjonctif présent", être ni kitenzi pekee kisichoishia na herufi "e" katika nafsi tatu umoja, na haibebi herufi "i" baada ya herufi "y" katika nafsi ya kwanza na ya pili wingi.

**Le quiz du week - end**

1. Kitenzi "Être" katika "Subjonctif" hunyumbuliwaje katika nyakati zilizowekwa hapo chini?

Subjonctif

Présent

Que je ...............

Que tu ...............

Qu'il/elle ...............

Que nous ...............

Que vous ...............

Qu'ils/elles ...............

Imparfait

Que je ...................

Que tu ...................

Qu'il/elle ...................

Que nous ...................

Que vous ...................

Qu'ils/elles ...................

Passé

que j' aie ............

que tu aies ............

qu' il/elle ait ..............

que nous ayons ...............

que vous ayez ..............

qu' ils/elles aient ...............

Plus - que - parfait

que j' eusse ...............

que tu eusses ...............

que il/elle eût ...............

que nous eussions ...............


que vous eussiez ...............

qu' ils/elles eussent ...............


**NB:** Katika "subjonctif présent" , être ni kitenzi pekee kisichoishia na herufi "e" katika nafsi tatu umoja, na haibebi herufi "i" baada ya herufi "y" katika nafsi ya kwanza na ya pili wingi.

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



A lichokifanya daktari

UNGEKUWA wewe ungefanyaje? Ebu msikie bibi huyu alipokuwa akipanda daladala.

**KONDA**: bibi twende siti kibao utalala

**BIBI:** oooh sawa mjukuu

**KONDA:** Simama tu, apo mbele wanashuka

Bibi akacheka

**KONDA:** Mbona unacheka bibi

**BIBI:** Mjukuu hawa wote hawashuki wote apo mbele watapata ajali.

**WATU:** Simamisha gari tuteremke.

SWALI

Ziwa Victoria liko ndani ya mikoa mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ndoa yako haijaanza kutikisika leo, ilianza tangu mwanzo wa uhusiano

KARIBU tena msomaji wangu, tuendelee kuelimishana kuhusu mitikisiko inayojiri kwenye familia zetu kila uchao. Maisha ni mtihani ambao kila mtu anapaswa kuupitia, japokuwa kwa mbinu tofauti.

Wiki iliyopita, tulimjadili mama anayekatazwa na mumewe kufanya kazi aliyoitafuta mwenyewe. Hata hivyo, hakukubali, akajitia nguvu akajisimamia na sasa anasonga mbele. Yamkini wako baadhi ya watu hukatisha wengine tamaa, lakini lazima ujitambue ujue haki zako za msingi. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mpenzi msomaji, yako mambo ambayo humtokea mtu katika maisha hadi anashangaa. Wakati mwingine anaishia kujilaumu au kulalamikia watu wengine asijue aanzie wapi. Lakini ukweli ni kwamba hakuna tatizo linalotokea kwa bahati mbaya kwani ni lazima kiwapo chanzo chake.

Kwa mfano, ndoa yako ina matatizo makubwa leo, jiulize, je, huko ulikoanzia wakati wa mahusiano ilikuwaje? Nini kilitokea? Ile picha au taswira uliyoiona mwanzo wa mahusiano au mwanzo wa ndoa, uwezekano ni mkubwa sana kujitokeza baadaye au mwishoni.

Kile kilichokuinua kilianza mwanzo. Kadhalika, kile kilichokuangusha kilianza mwanzo. Na ukweli ni kwamba pale unapokosea mwanzo, mwishoni utalipa gharama kubwa sana. Ukijenga nyumba isiyo na msingi imara, uwezekano ni mkubwa nyumba kubomoka.

Maandiko matakatifu yanasema msingi ukiharibika mwenye haki atafanya nini? Ukiona ndoa inatikisika leo, elewa kuwa msingi wake haukuwa imara, pengine ulikumbwa na sintofahamu nyingi ambazo hazikutiliwa maanani. Matokeo yake ndoa inavurugika, moja ya sababu kubwa ikitokana na viashiria vya awali.

Mama mmoja, mpenzi wa safu hii akaniambia baada ya kusoma moja ya makala za safu hii kwamba, "Ukiona mwanamume anamdharau mkewe, anamtukana au kumpiga, tabia hiyo haikuanza leo. Ilianza tangu mwanzoni mwa ndoa yao au pengine hata wakati wa mahusiano. Lakini si unajua pendo likichanganya hata ukipigwa unavumilia, kisa umempenda".

Akasema yeye yalimkuta wakati wa uchumba ambapo kila walipokuwa wanakwenda matembezini kwa mlo na viburudisho, mwenzake alikuwa hataki asalimiane na yeyote hata kama wanafahamiana. Akilazimisha lazima ugomvi mkubwa ulitokea mbele za watu.

Kingine akasema, hata alipopelekwa kwa wakwe kutambulishwa uchumba, mama mkwe, mawifi hawakumpenda. Na baada ya kuolewa ndio vituko vikaongezeka. "Ndipo nikagundua kuwa yale yaliyonitesa mwanzoni mwa ndoa ndio hadi leo nayashuhudia.

"Kibaya zaidi, mume wangu aliikimbia nyumba na kwenda kuishi na mwanamke mwingine. Ningetafakari yote yaliyokuwa yanatokea mwanzo wa ndoa yangu na kuchukua uamuzi sahihi, yote niliyopitia yasingenikuta", anasisitiza mama huyu.

Mpenzi msomaji, Mungu katika moja ya maandiko yake anasema, "Umeyaona mengi, umesikia mengi, lakini huyatilii maanani". Yamkini mtu anaona viashiia mbalimbali ambavyo havileti afya kwake, lakini anapuuzia. Jambo hili linatesa watu wengi sana na lina majuto. Ndipo mtu husema, "laiti ningelijua..., lakini kumbe ameshachelewa.

Ukitambua chanzo cha tatizo lako, ni rahisi kujua namna ya kulipatia ufumbuzi. Hata daktani unapomwendee, lazima ahoji chanzo, achunguze ndipo akupatie tiba. Hiyo ni kanuni ya kitabibu.

Kila tatizo la mwanadamu lina chanzo. Watu wengi wanahangaika na matokeo badala ya kutafuta chanzo. Mafanikio yoyote yana chanzo.Wapo waliofanikiwa sana hawajui chanzo.

Kila kitu kinachokupata kina sababu. Kuongelea matatizo ni kupoteza muda na kuhuzunika hakuondoi tatizo. Usipojua chanzo huwezi kutoka hapo ulipo. Lazima ukijue halafu ukiharibu ndipo utoke, usonge mbele. Ukitaka kukausha mti lazima uende kwenye mizizi. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Wapo watu leo ndoa zimesambaratika, kumbe chanzo ni asili ya kule alikotoka kwenye ukoo wake. Zipo familia wakioana wanaachana, yaani hawaoi wala hawaolewi. Usipozijua ukajitosa, matokeo yake ni majuto. Lazima uwe mdadisi tangu mwanzo.

Wengine wana roho za ulevi inayotawala familia.Wengine roho ya wizi. Ukichunguza utakuta yupo mwanafamilia alikuwa nayo, hivyo huo ni mnyororo unaopaswa kuvunjwa kupitia maombi. Hakuna kinachomshinda Mungu tunapomrudia na kumuomba, kwani anasikia na anatenda.

***Bila shaka msomaji wangu umejifunza jambo hapo. Kama una kisa, maoni ungependa tujadili pamoja, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. namba hii pia ipo WhatsApp. Tukutane wiki ijayo.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Misingi ya demokrasia ikiheshimiwa taifa litabaki salama

NI dakika za lala salama kwa Watanzania kufanya uamuzi wa maisha yao kwa miaka mitano ijayo.

Uchaguzi ndio utakaoamua wananchi wamemtaka nani awe diwani, mbunge na rais na hilo litafanyika kupitia sanduku la kura katika kukamilisha mchakato wa kidemokrasia kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania.

Tayari kampeni zimefanyika kwa wagombea kunadi sera zao, kueleza dhamira yao ya kuongoza kwa miaka mitano, kueleza ahadi zao na hasa kunadi ilani ambayo ndiyo mwongozo wa serikali watakayoiunda itakuwa ya aina gani.

Kwa kipindi cha siku 64 yamesikika mengi, yameandikwa mengi kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kwa ujumla.

Lakini kubwa ni baadhi ya Watanzania kupoteza maisha kuanzia kwenye mchakato wa kura za maoni na kampeni zenyewe,wengine wakijeruhiwa vibaya kiasi cha kuwa hospitali kwa muda mrefu na itawachukua muda mrefu kurudi katika hali zao za kawaida, na wengine wakiukizwa kisaikolojia kutoka na maneno ya kejeli, kuchafuliwa utu wao na kudhalilishwa.

Sasa tunakwenda kwenye kura yenyewe baada ya mashindano ya siku 64. Ni lazima ajulikane nani ni mshindi kwa mujibu wa matakwa ya wananchi pasipo kupendelea au kumbeba yeyote.

Nawaza kwa Sauti kuvisihi vyombo vya dola kutenda haki, kama kulikuwa na doa wakati wa mchakato wa kampeni basi zisionekane sasa ili kuondoa uwezekano wa kuvuruga amani.

Mamlaka za usimamizi wa uchaguzi kama Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zinajukumu la kuhakikisha nchi inavuka salama katika kipindi hivi.

Kumekuwa na makando kando mengi ambayo yamepigiwa kelele na wadau wa uchaguzi ambayo hayakutatuliwa kwa kiwango cha kuona kuna usawa kwa wachezaji wote wa timu.

Mathalani, katika hatua za awali kabisa wagombea wa vyama vya upinzani walienguliwa kwa madai ya kushindwa kujaza fomu vizuri na yapo majimbo ambayo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeshinda wabunge na madiwani wake wanasubiri kuapishwa.

Lakini duru za kisiasa zinahoji iweje vyama vya upinzani pekee ndiyo vikosee au iweje vyama hivyo tu ndiyo viwekewe pingamizi?

> **“Lakini wakati wa kampeni wagombea wa upinzani walifungiwa kufanya kampeni wengine ikiwa ni siku saba na 14. Pia wagombea udiwani walipigwa na kusekwa rumande kwa sababu tofauti tofauti.**

Lakini wakati wa kampeni wagombea wa upinzani walifungiwa kufanya kampeni wengine ikiwa ni siku saba na 14. Pia wagombea udiwani walipigwa na kusekwa rumande kwa sababu tofauti tofauti.

Pia duru zingine zinasema baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani walifika bei na ndiyo maana walikosea kujaza fomu ili kuruhusu mgombea wa chama tawala kupita bila kupigwa.

Kwa msingi huo, maana yake kasoro nyingi zimejitokeza na sasa ni wakati wa kila upande kurekebisha kwamba NEC na ZEC zisimamia uchaguzi kwa haki, kwa kuwa kiu ya wapiga kura ni kuona haki inatendeka kwamba yule waliyemchagua ndiye anakuwa kiongozi wao.

Wako wagombea walipata shida sana kujinadi kwa wananchi kiasi cha kukataliwa hadharani hiyo ni kutokana na sababu nyingi kama kutotimiza ahadi za mwaka 2015 na sasa wanarudi na ahadi zile zile.

Hii inaleta tafsiri kuwa wanatumia shida na umaskini wa wananchi kujinufaisha kwamba kwa miaka mitano hakuonekana kwa wapiga kura hadi miaka mitano imekwisha anarudi kwa watu wale wale kuomba awaongoze.

Uko ushahidi wa wazi juu ya nchi zilizopoteza amani kutokana na uchaguzi mkuu, nchi iligawanywa vipande vipande na watu wengi kupoteza maisha huku wengine wakibaki na majeraha makubwa ya kisaikolojia na mwili.

Ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha uchaguzi utuacha salama, ni wajibu wa mamlaka kutenda haki ili kusiwe na sababu yoyote ya kutokea vurugu.

Vyama vya siasa na husussan wagombea walifikirie taifa kwamba wasitangulize sana maslahi binafsi mbele bali yale ya wananchi wao, ni vyema kukubali matokeo yaliyotangazwa katika misingi ya haki, na kusiwe na usiginaji wowote wa kanuni ,taratibu na sheria.

Uchaguzi ni tukio la mara moja kila baada ya miaka mitano, lakini ndilo litakaloliacha taifa vipande vipande kiasi cha kuchukua miaka mingi kurejesha amani, maendeleo yote yaliyofanyika yanaweza kupotea kwa muda mchache ikiwa tu misingi ya demokrasia na haki haitazingatiwa.

***Mungu Ibariki Tanzania***

***Kwa maoni/ushauri salomekitomari33@gmail.com***

# HARUSI









Ilikuwa ni harusi ya kufana kati ya Elikunda Materu na mkewe Tonny John, iliyofanyika katika Kanisa la Celebration Church Dar es Salaam (CCD), Tarehe 18 Oktoba, 2020 na kufuatiwa na sherehe ya aina yake katika ukumbi wa Mwika Sinza, Dare s Salaam. PICHA: MIRAJI MSALA







# MITINDO











MAMA KIJACHO

## Magauni haya yanakufaa

KATIKA mila na desturi za Kiafrika, mwanamke mjamzito analazimika kuvaa nguo za staha na zenye maadili.

Nguo zinazopendekezwa kuvaliwa na mama mjamzito ni zile zenye ukubwa na urefu unaoweza kuficha maungo yake. Nguo za aina hizi humpatia uwezo wa kutembea au kufanya shughuli zake bila shida.

Hata hivyo, magauni yaliyotengenezwa kwa vitambaa vya pamba kama vitenge na khanga kwa kawaida yanatumia sana katika nchi za Kiafrika.

### VITU VYA KUZINGATIA

Magauni kwa ajili ya wanawake wajawazito lazima yazingatie ukubwa na urefu wa mvaaji, yasiwe yanabana au kupwaya sana kwani mama akiwa katika hali hiyo lazima aonyeshe urembo wake kama ilivyo huko nyuma.

Kwa wale wanaopenda kuweka mikanda au mipira juu ya tumbo, hakikisha inakuwa imara na yenye nafasi kwa mvaaji.

Chagua kitambaa ambacho hakisababishi joto, kitambaa cha pamba asilimia mia moja ni kizuri zaidi.

Angalia mtindo wa gauni kwanza kabla ya kuchagua, kama linaendana na mazingira na maadili ya kiafrika.

# UREMBO







## 'DREAD LOCKS'

# Nywele zinazoleta umaridadi

SIKU zinapozidi songa mbele, ndivyo watu wanavyoendelea kubuni na kuleta mitindo mipya ya usukaji na ukataji wa nywele.

Katika kipindi cha hivi karibuni, kumeibuka na aina mpya ya usukaji wa nywele aina ya 'Rock Dread' na kusababisha vijana kuchangamkia kwa kuanzisha saloon zinazohudumia aina hiyo ya nywele.

Mtindo huu wa nywele unaendelea kufanya vizuri tangu ulipoanza kuingia nchini, kundi linaloathirika na muonekano wa nywele za aina hii ni vijana na hasa wasanii na watu wengine maarufu.

Rock Dread ilianza kutumika katika nchi za Magharibi hasa Marekani, baadhi ya wasanii walionekana wakiwa na nywele za aina hii na wengine walinakshia kwa kuweka rangi mbalimbali.

Nywele za 'Rock Dread' zinapendeza zaidi kwa nywele fupi za asilia, kwani mtu akiwa nazo huwa anapendeza zaidi na hata kudumu kwake ni kwa muda mrefu.

Usukaji wa aina hii ya nywele inawahusisha watu wa jinsia zote.

**JINSI YA KUSUKA**

Rock Dread haisukwi kama mitindo mingine ya nywele, bali hutumika kifaa maalum ambacho kinasokota na kutengeneza aina fulani ya mawimbi makubwa au madogo.

Lakini kabla ya kusokotwa, unatakiwa kuhakikisha umekata nywele zako na kama mpenzi wa kupaka rangi, basi unatakiwa kufanya hivyo kwanza.

Ukimaliza, unapaka mafuta maalum ambayo hulainisha nywele, kisha unatumia kifaa hicho kwa ajili ya kutengeneza nywele zako.

# MAPISHI

## Na Mary Geofrey

# Jinsi ya kutengeneza tomato sauce



PISHI letu la tomato leo ni sehemu ya mahitaji ya nyumbani na familia kwa ujumla, unaweza kufanya biashara kwa kufungasha vyema na kutafuta wateja.

**MAHITAJI**

Nyanya kilo moja, vitunguu maji viwili, vinegar vijiko vitatu vya chai, sukari vijiko viwili vya chai.

Chumvi kijiko kimoja cha chai, maji ya moto kikombe kimoja cha chai na mafuta ya kula vijiko saba vya vyakula.

Haya ndiyo mahitaji ya kutaka kutengeneza tomato sauce, hata hivyo kama unataka kutengeneza zaidi ya hapo unatakiwa kuongeza uwiano wa mahitaji hayo.

**HATUA YA KWANZA**

Menya nyanya na vitunguu kisha vikate vipande vidogo vidogo, tumia brenda kusaga mchanganyiko wako.



Anza kuweka nyanya, vitungu, vinegar na sukari na katika brenda yako uanze kusaga kwa dakika kadhaa mpaka uone imetokea rojo laini.

**HATUA YA PILI.**

Tumia sufuria yenye nafasi kupika mseto huu. Weka sufuria yako jikoni tia mafuta ya kula acha yachemke kisha mwagia mseto wako na kisha uanze kukoroga kwa dakika 30 kuelekea upande mmoja huku ukichemka.

Baada ya hapo ipua mseto huo utakuwa umeshakuwa tayari.



# Bustani hupendezesha nyumba ikipangiliwa vizuri



ILI nyumba ipendeze zaidi inahitaji kunogeshwa na vitu tofauti ikiwamo bustani nzuri ya maua iliyotengenezwa kwa utaalam.

Mtaalam wa kutengeneza bustani ya maua eneo la Bunju B, Kinondoni Dar es Salaam, Mwagi Hassan, anasema utengenezaji wa bustani ya maua hasa katika eneo la nyumbani unahitaji ubunifu na utaalam mkubwa ambao wakati mwingine unahitaji kutumia akili nyingi.

Anasema ili uwe na bustani bora ya maua hatua za kuzingatia ni pamoja na kufahamu aina ya maua unayotaka kupanda, kama ni ya kudumu au ni ya muda mfupi.

Pili, anasema baada ya kuamua kuwa bustani yako ni ya aina gani, kinachofuata ni kuamua unayapanda kwa utaratibu upi, kama ni kwa mstari ulionyooka, duara, au kwa kufuata sura ya mchoro wa kitu chochote unachotaka wewe, mfano ramani ya Tanzania na nyinginezo.

Hassan anashauri kwamba katika upandaji wa maua, yapo yanayomudu juani na ya kivulini, hivyo ni lazima kufahamu mwelekeo wa vitu hivyo ili kutokuathiri ustawi wa bustani yako.

"Kwa mfano maua ya kuzunguka uzio, lazima upande kwa kufuata kipimo kinacholingana hata kama ni kamba, cha muhimu ni kuhakikisha kona moja na nyingine zinalingana ili wakati wa kupanda visipishane na unaweza kupanda maua zaidi ya aina moja ndani ya mstari uliochorwa," anasema Hassan.

Anashauri kwamba kama maua ni mapana, unapaswa kuyapa nafasi ya kutosha ili yapate hewa ya kutosha na nafasi ya kujitanua wakati wa kustawi.

"Na kama udongo wa uzio wako ni mgumu sana au una asili ya mwamba unatakiwa kujaza udongo mwingine kabla ya kuotesha chochote, weka na mbolea," anasema Hassan.

Anasema baada ya kutengeneza bustani yako na kupandikiza miche ya maua, ni lazima imwagiliwe kila siku kuanzia miche inapokuwa midogo hadi mizizi yake inapochipua na baada ya hapo umwagiliaji wake utategemea na aina ya udongo na hali ya hewa.

## MPANGILIO

# Dondoo muhimu za kuandaa eneo la kupumzikia katika bustani


**1:** Unaweza kuweka viti viwili na meza katika bustani yako ndogo kwa ajili ya kukaa nyakati za jioni au asubuhi.

**2:** Katika bustani unaweza kujenga kibanda ambacho ndani yake weka viti viwili na meza ndogo.

**3:** Weka matairi au mawe juu ya maua ambayo yatatumika kama sehemu ya kupumzikia.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NIMEKUNADI SANA NIMEZUNGUKA KILA PEMBE KUKUOMBEA KURA, ILA SIKUWA NA MAJIBU KAMA WAKI-KUPA UTAWEZANA? KAJIBU WEWE
'USHANIUA' BADO KUZIKWA TU!
KAMPENI ZA LALA SALAMA MKE WANGU NIMEJIONGEZA TU!
NDIO UTUMIE MUDA WAKO WOTE JUKWAANI KUSIFU WANAWAKE BADALA YA KUNADI SERA? ILI IWE NINI KAMA SIO UZINZI?
JIHESABU 'UMESHAPITA' LICHA YA MIKUTANO YAKO YOTE KUJAZA WATOTO BADALA YA WATU WAZIMA.
KWA HIYO WALIKWENDA KUWASAMBAZIA WAZAZI WAO SERA ZANGU?
MUNGU ANAKUONA
JITAHIDI ACHA POROJO FYATUA SERA ZA NGUVU ZINGINE ZIBUNI PAPO KWA PAPO SIKU ZIMEISHA
SAWA, LAKINI NA WEWE PITAPITA KWA WATAALAMU KUONGEZA NGUVU
HATA SIKU MOJA UJAJITOKEZA KUWASIKILIZA WAGOMBEA.... UTAWEZAJE KUPIGA KURA!
WEWE HUKOSAGI MIKUTANONI KWA AJILI YA 'MONDI NA KONDEBOI' NAMBIE UTAMPIGIA NANI KATI YAO?
SIJAJUA TATHIMINI YA KUJINADI MBELE YA WAPIGA KURA KAMA WAMENI-KUBALI, AU NIME-CHOMA MAFUTA ILI NIJUE CHA KUWAFANYA
KWA ZILE SERA ZAKO ZA KILA MKULIMA ATAVAA SUTI SHAMBANI "UMEPITA BILA KUPINGWA"
UPITE HIYO KWIO?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPENDA KUBEBWA KUMBUKA KUFUA MBELEKO...

HABARI KIMATAIFA

# Kauli ya Papa yaleta mgongano Katoliki

**VATCAN, Italia**

SIKU chache baada ya kiongozi wa Kanisa la Katoliki Duniani, Papa Francis, kutoa maoni ya kuwatambua wapenzi wa jinsia moja, baadhi ya makadinali wamejitokeza kupinga kauli hiyo.

Mmoja wa makadinali hao, Raymond Burke, alijitokeza na kusema kauli hiyo ni maoni binafsi Papa na hayastahili kufuatwa na Wakatoliki.

Burke ambaye amekuwa mkosoaji mkubwa wa kiongozi huyo mwenye mlengo wa kihafidhina,alisema pendekezo la Papa Francis la kutaka ndoa ya wapenzi wa jinsia moja kutambuliwa kisheria halijawashangaza wengi, lakini maneno aliyotumia ndio yaliyowashangaza viongozi wa kidini na waumini wa Kanisa Katoliki.

Kadinali huyo alitaja kauli ya Papa kama maoni kibinafsi, na kwamba Kanisa katoliki na waumini wake hawatashurutishwa kutii msimamo wa kiongozi huyo wa juu wa Kanisa hilo.

Aliwataka viongozi wa kanisa hilo kutoa maelekezo ya kina kama jukumu lao lililobakia.

Kadinali Burke alisema imani rasmi ya kanisa ni kutotambua ndoa ya wapenzi wa jinsia moja, hivyo kauli hiyo ya Papa imewahuzunisha waumini wengi.

Mafundisho ya Kikatoliki yanaeleza uhusiano wa wapenzi wa jinsia moja ni kama tabia potofu.

Katika kauli yake, Papa Francis alisema anafikiria wapenzi wa jinsia wanastahili kuruhusiwa kuwa na familia.

"Watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja wana haki ya kuwa na familia,"alisema.

Aliongeza kusema katika filamu inayoelezea maisha yake "Ni watoto wa Mungu wana haki ya kuwa na familia.

Hakuna mtu anayestahili kutengwa au kufanywa ajihisi mnyonge kwa kuamua kuwa katika uhusiano wa aina hiyo,"

Filamu ya Francesco, inayoelezea maisha na kazi za Papa Francis, ilionyeshwa hivi karibuni katika Tamasha la Filamu la Roma

Baadhi ya wataalamu walisema tamko la Papa Francis, linaendana na msimamo unaoungwa mkono na maaskofu wengi duniani, lakini kinachotofautiana ni viongozi hao wanakubali kuhusu ulizi wa kisheria wa wapenzi wa jinsia moja na wala sio kuhalalisha ndoa.

Hata hivyo, wachambuzi wengine walisema matamshi ya Papa Francis, hayakuidhinisha ndoa ya wapenzi wa jinsia moja kama watu wengi wanavyoamini.

**BBC**



Madereva wa teksi wakizuia barabara kwa magarai yao kupinga uendeshaji wa kampuni ya usafirishaji abiria Uber katika jiji la Bogota, nchini Kolombia. **(PICHA: AFP)**

# Amani Libya yakaribia kupatikana

**TRIPOL, Libya**

PANDE mbili zinazopigana nchini Libya, zimetiliana saini mkataba wa kudumu wa makubaliano ya kusimamisha vita baada ya kufanyika mazungumzo ya siku tano yaliyosimamiwa na Umoja wa Mataifa.

Makubaliano hayo ya kihistoria yamefikiwa baada ya majeshi ya serikali na vikosi vya waasi kuwa katika mapigano tangu kuawa kwa aliyekuwa Rais wa Nchi hiyo Muhamar Gaddaffi mwaka 2011.

Katika makubaliano hayo, pande zote mbili zinatakiwa kuondoa mamluki kutoka nje na kuweka mazingira ya mazungumzo yatakayofanyika mwezi ujao.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alisema makubaliano yaliyofikiwa ni jambo la muhimu, na kuhimiza juhudi zaidi zinahitajika kuleta amani nchini humo.

Mjumbe mwandamizi wa umoja huo, anayeshughulikia mgogoro wa Libya, Stephanie Williams, alisema vikundi vyenye silaha na vikosi vya kijeshi vimekubali kurejea kwenye kambi zao mara moja.

Shirika la Mafuta la Kitaifa la Libya (NOC), limetangaza kuanza tena shughuli za usafirishaji wa mafuta kutoka kwenye vituo viwili muhimu mashariki mwa nchi hiyo mara baada ya pande hizo kutiliana saini.

**DW**

## Waandamanaji 51 wauawa Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

IDADI ya watu waliouawa katika maandamano yaliyoambatana na vurugu nchini Nigeria, imefikia 51 kulingana na ripoti iliyopatikana jana.

Maandamano hayo ambayo yamedumu kwa muda wa wiki moja, yalitokana na madai ya vijana ambao walipinga ukatili wa kikosi maalumu cha Polisi cha kupambana na ujambazi kinachofahamika kama Sars.

Kwenye maandamano hayo, askari 11 pia wamethibitika kuuawa na raia wengine 37 wamejeruhiwa.

Rais Muhammadu Buhari, aliewalaumu wale aliowaita wahuni kwa kusababisha machafuko hayo, huku akisisitiza vikosi vya usalama vilijizuia kwa kiwango cha juu kupunguza athari.

Buhari aliongeza kuuwa maandamano hayo yaliyokuwa na nia njema, yalitekwa na majambazi walioyaingilia kati. Hata hivyo, kauli ya Buhari ilionekana kuendeleza mivutano zaidi.

Wanigeria wengi wamekasirishwa na hotuba ya Buhari, aliyoitoa siku ya Alhamisi usiku, baada ya kukosa kutaja vitendo vya ukatili vya wanajeshi wake ambao waliwafyatulia risasi raia.

Badala yake kiongozi huyo aliwaonya waandamanji dhidi ya kuhujumu usalama wa kitaifa, sheria na utulivu.

**DW**

## Ethiopia yaonya vitisho ujenzi wa bwawa la umeme

**ADIS ABABA, Ethiopia**

ETHIOPIA imesema haitokubali vitisho vyovyote na majirani zake ambao wanataka kusimamisha mradi wa ujenzi wa bwawa kubwa la umeme.

Ofisi ya waziri Mkuu wa nchi hiyo, Abiy Ahmed, haikumshutumu mtu au nchi yoyote katika taarifa hiyo ambayo inaelezea maendeleo ya bwawa hilo la Grand Renaissance, ambalo limejengwa katika mto Nile.

Kauli hiyo imetolewa saa chache, baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump, kufanya mazungumzo kwa njia ya simu na Waziri Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, na kutoa wito wa suluhu wa irafiki kati ya Ethiopia na Misri.

Katika maongezi hayo yaliyofanyika mbele ya waandishi habari katika ikulu ya White House, Trump alisema ameipa Misri ushauri kama huo na kuongeza kuwa hali imekuwa ya hatari.

Aidha Rais Trump alionya Misri inaweza kulilipua bwawa hilo.

Ethiopia, Sudan na Misri zimekuwa katika mgogoro mkubwa kuhusu ujezi wa bwawa hilo.

**DW**

## MAKALA

# Uamuzi wetu utaamua amani yetu



Na Magabilo Masambu

ZIKIWA zimesalia takribani siku mbili kufikia Oktoba 28, 2020 ambapo Watanzania watatimiza takwa la kikatiba la kuwachagua viongozi wao kwa njia ya kidemokrasia, joto la uchaguzi mkuu linazidi kupanda kila kukicha.

Amani inawezekana ndilo jambo linalozungumzwa zaidi na Watanzania, lakini pia wasio Watanzania kwasababu amani ya Tanzania ni msingi mkuu wa amani ya majirani zetu pia. Kila kona ya nchi kuna kelele nyingi sana zinazohusu amani ya nchi yetu kuelekea siku ya uchaguzi na baada ya uchaguzi.

Hofu kubwa inaonekana mioyoni mwa Watanzania wengi jambo ambalo ni la kawaida panapotokea jambo ambalo hudhaniwa kuwa si la kawaida.

Uchaguzi wa mwaka huu 2020 kama tunavyofahamu si uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi ni uchaguzi wa sita, lakini ni uchaguzi unaoonekana kuwa na vuguvugu na ushindani mkali kati ya vyama viwili pengine hili ndilo linaloleta hofu kubwa na kutulazimu kila kona ya nchi kuimba wimbo mmoja wa amani yetu.

Jambo la kulinda amani ya nchi hii na hasa kuelekea siku ya uchaguzi mkuu ni la kila Mtanzania, wenye mamlaka na wasio nayo, kwasababu amani ikivunjika haitavunjika kwa upande mmoja tu ni jambo litakalo tuhusu sote hivyo kila mmoja lazima ahakikishe amani inakuwa kipaumbele kwa kusema na kutenda yaliyo mema.

Kama wasemavyo wengi kwamba hatuwezi kutenganisha Amani na Haki zinapovunjwa haki za watu inasababisha kuvunjika kwa amani ya watu vilevile. Kwahiyo wale wote walio katika nafasi ya kutenda haki wanajukumu kubwa la kuilinda amani ya nchi hii kuliko watendewa haki wenyewe.

Wakati huu kila uamuzi unaofanywa na yeyote lazima yawe yametazamwa ni kwa kiasi gani yanaweza kuleta heri au shari! Kwa kuwa uamuzi yetu ndiyo utaamua amani yetu. Tunafahamu kwamba nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria na ziliwekwa ili kulinda haki mbalimbali za watu, maana yake ni kwamba kama hatutaendesha mambo kwa kujali sheria au wanaostahili kuzifuata kama hawatafuata basi haki za baadhi yetu zitavunjwa na zikivunjwa na amani pia inavunjika.

Uchaguzi mkuu ni muhimu sana, lakini muhimu zaidi ni amani yetu kwasababu ikiwa uchaguzi utafanyika na viongozi wakapatikana wanahitaji kuongoza watu sasa amani ikivunjika na viongozi wakapatikana watawaongoza akina nani? Ni jambo tunalopaswa kujiuliza kabla ya kutenda chochote ili tuvuke salama katika kipindi hiki.

Tume ya Uchaguzi, vyombo vya usalama,wagombea na wananchi wote tunajukumu la kuhakikisha amani ya nchi yetu inaendelea kutamalaki kwa kufuata sheria zetu na hasa za uchaguzi pamoja na nyingine za nchi tukizifuata na kuzitii tutavuka salama. Nchi hii ni yetu sote hakuna mwananchi bora zaidi ya mwingine kila mmoja ana nafasi sawa na mwingine kwa ubinadamu wake.

Tuwaonee huruma watoto, wazee, wenye ulemavu, kinamama ambao mara nyingi ndiyo waathirika wakubwa amani inapovunjika. Tanzania kwa miongo kadhaa tumekuwa msaada mkubwa kwa majirani zetu wanapopata matatizo ya ukimbizi baada ya amani katika nchi zao kuvurugika, litakuwa jambo la ajabu sana kama baada ya uchaguzi nasi tutafanana nao. Tuilinde heshima ya nchi yetu tunatazamwa na wengi ambao wanasubiri kwa hamu ili siku moja tusiwe washauri tena.

Bado tuna matumaini makubwa na vyombo vya maamuzi pamoja na changamoto zilizopo kwamba haki itaendelea kutendeka ili uchaguzi upite salama na kuwapata viongozi watakao tuongoza katika awamu nyingine. Kuhubiri amani pekee bila haki ni sawa na kuhubiri pepo bila kutubu dhambi, turekebishe kasoro zinazojitokeza wakati huu wa mchakato ili siku ya uchaguzi tuwe na amani ya kutosha na baada ya matokeo ziwe furaha na vifijo kwa wale watakaokuwa wamechaguliwa.

Sisi ni ndugu, kaka na dada, hakuna sababu ya kuvurugana, tunahitajiana sote kwa namna mbalimbali, tukipendana hatutaumizana kwasababu sio tabia za kitanzania. Niwatakie uchaguzi mwema naimani tutavuka salama.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Bruce Lee alivyosababisha watu wapigane kifua wazi



Na Adam Fungamwango

MIAKA ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1980, hakukuwa na mwigizaji mkuu maarufu kama 'sterling' aliyeheshimika na kupendwa zaidi kwenye sanaa za mapigano kama Bruce Lee.

Ndiye aliyeaminikia kuwa binadamu aliyekuwa fiti zaidi kuliko mwingine yoyote yule.

Aina yake ya uchezaji wa filamu, staili yake ya kupigana iliwafanya wazee wengi wakati ule, vijana na hata watoto kumkubali.

Ndiye sterling aliyekuwa na mashabiki wengi zaidi kuliko wengine, iwe wa Kichina, Kizungu, Kijapani au wa Kihindi.

Bruce Lee, kijana wa Kichina wakati huo, aliyezaliwa nchini Marekani na kupata uraia wa huko na hata alipofariki dunia mwaka 1973 alizikwa nchini Marekani, baada ya kufia kwenye nchi yake ya asili China.

Hadi leo hii, bado kuna mashabiki wa sinema wanaamini kuwa hakuna 'sterling' yoyote yule mwenye uwezo wa kupigana kama Bruce Lee.

Hadi anafariki dunia, Bruce Lee alikuwa ametoa filamu tano tu kali ambazo ni 'Big Boss', 'Fist of Fury', 'The Way of Dragon', 'Enter the Dragon' na 'Game of Death'.

Ni filamu hizo tu ndizo zilizomfanya kijana huyo ambaye alifariki akiwa na miaka 32 tu kuwa staa mkubwa zaidi duniani kwenye sanaa za mapigano, ingawa huko nyuma alitoa baadhi ya filamu ambazo hakuwa maarufu duniani.

Bruce, aliyezaliwa Novemba 27, 1940 kwenye hospitali ya Wachina, San Francisco, California nchini Marekani na kufariki dunia Julai 20, 1973 alikuwa maarufu sana kwa staili yake ya mapigano ya 'kung-fu', ambaye mwenyewe aliibatiza jina la 'Jeet Kune Do.'

Watanzania wengi ambao walianza kuziangalia picha za Bruce Lee katikati ya miaka ya 1970, walifanya hivyo wakati Bruce mwenyewe akiwa ameshafariki dunia.

Hii ina maana kuwa Bruce Lee kwa asilimia kubwa umaarufu wake ulikuja wakati yeye mwenyewe akiwa kaburini. Hata filamu zake hizo zilianza kutoka miaka michache tu kabla ya kifo chake na zingine zikitoka baadaye ya yeye kufariki.

Ni kweli nchini Marekani na China alishaanza kuwa staa, lakini ustaa wake waliposambaa duniani na kila mtu kumkubali kuwa huyu ni mfalme ya 'kung fu', tayari alikuwa ameshafariki dunia.

Pia wakati huo nchini Tanzania filamu zilikuwa zinachelewa sana kufika, tofauti na sasa ambapo teknolojia imekuwa, filamu inaweza kutoka leo na leo hii ikaanza kuonekana dunia nzima.

Miaka hiyo filamu zilikuwa zinafika nchini baada ya kuzunguka sana duniani. Ya mwaka 1970 inaweza kufika hata baada ya mwaka mmoja au miwili, kutegemea umaarufu wa picha yenyewe. Na filamu yenyewe ni mkanda mrefu unaokuwa amezungushwa na kuwekwa kwenye maboksi.

Na hata ukiingia nchini ni huo huo mmoja tu ndiyo inakuwa unazungushwa kwenye kumbi mbalimbali za kuonyesha filamu na baadaye huo huo unaanza kusafirishwa mikoani.

Hii ni tofauti na sasa ambapo kila nyumba chini inaweza kuwa na nakala ya filamu ya 'Big Boss'.

Filamu la kwanza iliyofanya hata mashabiki duniani kushtuka na kuanza kumuangalia kama mmoja wa wapiganaji wa hali ya juu ni 'Big Boss'. Ni filamu yake kali ya kwanza iliyotoka mwaka 1971 na kukonga nyoyo za mashabiki wa picha za mapigano wakiwamo Wabongo.

Mwaka 1972, alitoa picha mbili kali ambazo ni 'Fist of Fury' na 'The Way of Dragon'.

Filamu ya 'The Way of Dragon' ilijulikana hivyo nchini China na huku Tanzania, lakini Marekani ilijulikana na 'Return of the Dragon' ambayo Bruce Lee alipigana na bingwa wa karate wakati huo nchini Marekani, Chuck Norris. Mwaka 1973 ambao Bruce Lee alifariki dunia ndipo filamu yake kali kabisa 'Enter The Dragon' ilipotoka.

Ni kwamba Bruce alifariki kabla filamu hii haijatoka. Ina maana yeye mwenyewe hakuiona ikiwa tayari inaonyeshwa. Baada ya kuicheza filamu huu, alifariki akiwa bado yeye na wenzake wanaihariri.

Ilitolewa rasmi Agosti 19, 1973, wakati akiwa amefariki dunia, Julai 20 mwaka huo huo. Ina maana ilitolewa mwezi mmoja baada ya kifo chake. F ilamu hii aliicheza nchini Marekani akiwa na mastaa wengine wakali wakati huo kama Angela Mao, John Saxon, Jim Kelly na wengineo.

Kuna filamu nyingine ya 'Game Of Deth' Hii inadaiwa ilichezwa na kutengenezwa na Bruce Lee mwenyewe mwaka 1972 lakini ilikuwa bado haijatolewa sokoni. Hata hivyo ilikuja kutolewa mwaka 1978, miaka mitano baada ya mwenyewe kufariki dunia.

Pia 'Game of Death' ziko mbili. kuna namba moja na namba mbili. Namba moja yote ilichezwa na Bruce Lee, lakini namba mbili Bruce Lee aliishia kati kwani alifariki kabla hajaimalizia.

Sehemu iliyobakia aliicheza kijana mmoja Mkorea, Kim Tai Jong ambaye alimalizia vipande vyote vilivyobaki ambavyo alikuwa acheze Bruce Lee na alifanya hivyo kwa umahiri mkubwa.

Ni wale wajuzi tu wa mambo ndiyo wanaoweza kutambua kuwa anayepigana si Bruce Lee, lakini si wengi wakiangalia filamu hiyo iliyotoka mwaka 1981 wanaoweza kugundua tofauti yoyote ya muonekano, wajihi na aina yake ya mapigo kana kwamba ni Bruce.

Amefariki dunia lakini aliwaachia vijana wa Kitanzania wakati huo ujasiri mkubwa. Wengi walitaka kuwa kama yeye. Wengi walivutoka kujifunza karate na 'kung fu' kama vijana wa sasa wanavyopenda kujifunza bongo fleva. Iliwafanya vijana wengi wakati hio kuwa wakakamavu kwani kila mmoja alipenda kuwa kama Bruce Lee.

Hata wakati wa kupigana wakati huo, kila mmoja alipenda kuvua shati kama anavyofanya Bruce Lee. Ukiangalia filamu zake nyingi mwamba huyu ni kwamba anapigana kifua wazi, hasa zile sehemu za mwisho anapopigana na watu wenye uwezo mkubwa unaotaka kulingana na yeye.

Huyu ndiye Bruce Lee, mbabe, stelingi wa sanaa za mapigano anayebaki kuwa ndiye staa wa karne ya 20 kwenye filamu za aina hiyo kuliko yoyote yule aliyepata kutokea duniani.

Hata alipofariki dunia, wengi hawakuamini kuwa mtu mwenye nguvu na uwezo wa aina hiyo anaweza kufa ghafla hivyo. Ukweli ni kwamba Bruce Lee licha ya kwamba vile anavyovifanya anaigiza filamu, lakini ukweli ni kwamba ndivyo alivyo.

Bruce Lee alikuwa binadamu aliyejaaliwa nguvu na uwezo mkubwa na kupigana kiukweli kabisa ukiondoa vile anavyofanya kwenye filamu. Inasemakana kuna wakati alikuwa akiwaumiza wenzake kwenye kuigiza.

Kutoamini binadamu huyo 'nusu mtu nusu chuma' anaweza kufa ghafla hivyo, ndiyo ikasababisha habari nyingi za uvumi kutokana na kifo chake.

Mara alinyweshwa sumu na mwanamke. Mara ilikuwa njama za Wachina kumuua kutokana na kuwa alikuwa mwalimu wa kuwafundisha Wamarekani mchezo huo hasa wacheza filamu, wakati wao walitaka uwe wao tu. Ili mradi tu kila mtu alikuwa akiongea lake. Lakini ukweli ukabaki pale pale kuwa Bruce Lee alikuwa amefariki. Hakuna wa kulaumiwa. Aachwe aendelee apumzike kwa amani kwenye kaburi lake nchini Marekani.

HADITHI

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka, na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Sesilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-5

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

HALI ya Magdalena Rupia, mama mzazi wa Cecilia ilibadilika tena. Akapelekwa kimbizwa tena kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

Huko ilibidi atundikiwe 'dripu' na kulazwa. Cecy na ndugu zake kina Badaka kama kawaida, mchana walikuwa na zamu ya kupeleka chakula, na jioni kwenda kumtazama mgonjwa.

"Zahir mama amelazwa kwenye Hospitali ya Mwananyamala." Ilikuwa ni sauti ya Cecy, akiwa amekaribia kufika kwenye geti la hospitali, akimpigia simu mpenzi wake.

"Ahaaa, mhh, poleni sana."

"Sasa wewe uko wapi uje huku?"

"Ohh, samahani siwezi kuja kwa sababu sipo Dar es Salaam."

"Mhh, mbona hujaniambia kama unasafiri?"

"Ilikuwa ghafla sana."

"Jana tuliongea kwenye simu usiku mbona ulikuwa Dar?"

"Ndiyo, lakini niliondoka alfajiri, niko Morogoro kikazi. Ngoja baadaye nitakutumia laki mbili kwa ajili ya mgonjwa."

Cecy hakujibu kitu. Alibaki kama bubu.

"Zahir hayupo Dar eee." Sauti ya Badaka ilimshtua.

"Ndiyo, kaniambia hivyo."

"Ngoja nimpigie shemeji yangu wa zamani, nimwambia mama amelazwa. Huyu wala hana tatizo, atakuja tu." Badaka alisema akimwangalia kwa madaha dada yake.

Cecy, hakutaka kujibu chochote. Moyo ulimsuta. Hakuhitaji pesa. Alichohitaji ni faraja ya moyo wake. Alichohitaji ni mpenzi wake aje kumuona mama yake. Anakumbuka hata mara ya kwanza wakati mama yake alipolazwa hakufika pia.

Alituma pesa tu na kuendelea na shughuli zake. Lao anasema yuko safari. Anakumbuka aliyekuja ni Mashaka ambaye wakati huo alikuwa hajui kuwa penzi lake tayari lilikuwa limeshaingiliwa na Zahir, akaishia kumtukana.

"Mambo Mashaka."

"Nzuri tu Badaka."

"Shemeji yangu nakuarifu tu kuwa mama amelazwa tena."

"Duh, poleni sana, nitafika basi jioni kumuona."

"Njoo tu shemeji yangu, usihofie chochote, hutopata matatatizo tena kama yale."

"Haya nashukuru."

"Kasema anakuja jioni." Badaka alimpasha dada yake ambaye alibaki kimya kama mtu mwenye mawazo.

Ilipofika saa 10 jioni, Mashaka alitimba hospitalini kama kawaida yake. Safari hii alikuwa amebeba soda.

Mwenyeji wake alikuwa Badaka. Ingawa alimsalimia Cecy, hakutaka kuwa karibu naye. Aliogopa vijembe na maneno ya kejeli ambayo amekuwa akiyatoa siku za karibuni kwake.

Aliogopa kusemewa ovyo mbele ya kadamnasi ya watu. Anamfahamu vilivyo Cecy. Lakini pia anakumbuka maneno ya mwisho aliyoambiwa.

"Nachokwambia ni hivi, kuanzia leo ukome kunifuatilia. Mimi si mpenzi wako tena, futa hilo wazo kwenye kichwa chako, na kuanzia sasa tukimaliza hapa mimi nafuta namba zako, na wewe futa zangu." Alikumbuka maneno aliyoambiwa kwenye simu siku ile.

"Shemeji mimi nimekuja mara moja tu kumwona mgonjwa, kuna sehemu naenda muhimu, nadhani nikipata nafasi kesho nitakuja tena kumuona," alisema Mashaka baada ya kumkabidhi mgonjwa soda.

"Badaka, huyu ni nani, hii ni mara ya pili kama sikosei namwona anakuja hapa hospitalini." Mama Badaka alimuuliza binti yake kwa sauti ndogo na hafifu.

"Mhh! Mama yaani pamoja na kuumwa kote unawakumbuka hata wanaokuja kukuona?"

Mama alitabasamu kwanza "Namkumbuka huyu kijana aliwahi kuja tena nilipolazwa kwa mara ya kwanza, tena ulikuja naye wewe kama hivi leo, niambie binti yangu nani huyu?"

Si wengi walioyasikia sana maneno hayo kwa sababu mgonjwa aliyasema kwa sauti hafifu ya ugonjwa, kiasi kwamba aliyekuwa akiyasikia kwa ufasaha ni mwenyewe aliyekuwa akiulizwa ambaye ni Badaka.

Cecy pia aliyasikia. Kwa mbali alihisi kama aibu hivi. Alibaki kando bila kusema kitu chochote. Macho yake yalimwiba Mashaka, akawa anamwangalia kwa chati. Mashaka aligeuka akiwa kama anaondoka. Hakutaka kusikia zaidi maneno ya mama kwa aibu.

"Kama ni mkwe wangu, basi Badaka ujue umepata mwanaume anayejali, kama bado hajawa mkwe wangu, basi hebu mwangalie. Ni kijana mzuri. Si vijana wote wenye moyo kama huu. Kuja tu kuniangalia kunatosha sana. Huyo dada yako Cecy sijaona hata mtu mmoja kuja kuniona. Unafikiri atakuwa hana, si kweli. Sijaona amlete mtu hapa."

Badaka aligeuka na kumtazama dada yake. "Mama Angejua" Alijisemea moyoni.

Cecy alionekana kama mgonjwa. Alikuwa ameinama chini. Alionekana kama mwenye hatia. Hakumtazama Badaka wala mama yake.

Taratibu Badaka alichukuzana na shemeji yake Mashaka na kutoka ndani ya wodi ya wanawake kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

"Mhh! Mama naye. Yaani anaona kama mimi wewe ndiyo mpenzi wangu."

"Ndiyo, kwa sababu siku ile dada yako aliponifukuza wewe ndiye ulinichukua na kunileta. Leo tena ananiona na wewe. Unadhani atahisi vipi?" Mashaka alidakia.

"Akija kujua atashangaa kweli."

"Labda wewe ndiyo umwambie. Lakini vipi dada yako si atakuwa na mwanamume hivi sasa?"

"Shemeji nikwambie ukweli tu, yule anaye, lakini mimi simjui, maana wanaitana kwenye simu, sijawahi hata kushirikishwa. Ila nasikia jamaa ana pesa kweli, ila kwa siku za karibuni naona kama dada hana furaha hivi. Mapenzi na pesa shemeji ni vitu viwili tofauti, japo vyote vinatakiwa."

*****************************

"Zahir unasikia, unanitia aibu mimi mbele ya ndugu zangu na watu wanaonizunguka."

"Kwa nini unasema hivyo Cecy."

"Haiwezekani kaka zangu wanakwenda hospitalini na wake zao, wapenzi wao kumuona mama, mpaka mdogo wangu Badaka naye anakuja na mpenzi wake, mimi nakwambia njoo na mimi nionekane wa maana wewe unakataa. Wewe utakuwa hunipendi."

"Nakupenda ila niko bize mpenzi wangu."


"Siyo kweli, jana nilionana na rafiki yako Mussa, akaniambia hujasafiri wala nini, ulikuwa hapa hapa Dar."

"Huyo Mussa ulikutana naye wapi? Au anakutaka, anaanza kuleta fitina ili akuchukue?"

"Yaani ushaniona mimi najiuza eee? Nitoke kwako, halafu nikamchukue na rafiki yako, yaani umenichoka kweli."

"Lakini mpenzi, pesa si nilikutumia shilingi laki mbili kwa ajili ya mama?"

**INAENDELEA JUMAPILI**




"Kama ni mkwe wangu, basi Badaka ujue umepata mwanaume anayejali, kama bado hajawa mkwe wangu, basi hebu mwangalie. Ni kijana mzuri. Si vijana wote wenye moyo kama huu. Kuja tu kuniangalia kunatosha sana. Huyo dada yako Cecy sijaona hata mtu mmoja kuja kuniona. Unafikiri atakuwa hana, si kweli. Sijaona amlete mtu hapa."



# KASILIMU

## *Ben Pol sasa ustaadhi Benham*

KATIKA hali isiyotarajiwa, mwanamuziki mahiri wa RnB nchini, Ben Pol, amebadilisha dini na sasa amekuwa muumini wa imani ya Kiislam.

Msanii huyo jana aliposti picha kadhaa akiwa amevaa kanzu akiambatana na Sheikh Issa Othman Issa, imam wa msikiti wa Maamur uliopo Upanga jijini Dar Es Salaam.

Aidha msanii huyo alionyesha cheti chake ambacho kilionekana jina lake jipya kuwa ni Benham Paul Mnyanganga, badala la lile la awali la Benard Paul Mnyanganga.

Baadhi ya mastaa wamejitokeza kumpongeza kwa hatua yake hiyo akiwamo Ommy Dimpoz, Fid Q, Mwana Fa

## Tupac Shakur wa Bongo huyoo!

MWANAMUZIKI anayechipukia, Ice Boy, amesema maisha yake hayapo kwa kuwaigiza wasanii wa Marekani, badala yake kila kitu anachokifanya kinatokana na uhalisi.

Ice Boy ambaye anafananishwa na marehemu Tupac Shakur, amesema kuwa pamoja na kufanana na rapa huyo, lakini hamtukuzi kama wanavyofanya wengine.

"Mimi ndiyo msanii ninayevaa zaidi Africa, hapa Bongo nipo kwa makusudi kwa sababu nipo tofauti na wote kabisa maana ningezaliwa Ulaya ningefanana na watu wengi, mimi sijifananishi na Tupac ila nafanana naye na sijawahi kumpost kwenye page yangu, siigizi wala sijifananishi naye kwa chochote ila nafanana naye" amesema Ice Boy



## Dah! Steve Nyerere kashtuka bhana

SUALA la msanii wa filamu za Bongo Muvi, Wema Sepetu, kuonekana kuwa karibu na mchezaji wa Yanga Corlinhos, sasa limechukua sura mpya baada ya mwigizaji Steve Nyerere, kutilia shaka ukaribu huo.

Steve aliandika katika ukurasa wake wa Istagram kwamba binafsi anaona kama Wema anafanya hujuma kwa Timu ya Yanga ambayo anaipenda.

"Uongozi wa Yanga popote mlipo mtatuua mashabiki wenu jamani, tunanunua mchezaji kwa bei kubwa, tunampokea uwanja wa ndege kwa mbwembwe, dakika ya mwisho hali ndiyo hii, tafadhali kuhujumu uchumi sio kuiba hela tu hata hili mnaloliona, kuna watu watawajibika Wema Sepetu endelea nakwambia" ameandika Steve Nyerere



# Guardiola: Koeman ahitaji muda zaidi Barca

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini Ronald Koeman "anahitaji muda zaidi" kuifanya Barcelona icheze namna anavyotaka yeye.

Guardiola na Koeman walikuwa wachezaji wa Barcelona, kabla ya kuachana mwaka 1995 wakati Koeman alipokwenda Feyenoord.

Na wawili hao walibakia kuwa marafiki na Guardiola alimtaka Koeman kurudi Barcelona baada ya msimu mbaya wa 2019-20.

Jana Jumamosi, Koeman aliiongoza kwa mara ya kwanza Barcelona kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya Real Madrid kama kocha, na kumfanya kuwa kocha wa saba raia wa Uholanzi kuwanoa miamba hao wa Katalunya kwenye mchezo huo maarufu wa LaLiga.

Na Guardiola, ambaye aliiongoza Barcelona kutwaa mataji 14 katika miaka minne kutoka 2008 hadi 2012, anaamini muda utamsaidia Koeman kuifanya timu hiyo kuwa kwenye kiwango chake.

"Wakati mwingine unahitaji muda zaidi ili kupata kila kitu," alisema Guardiola.

"Hasa kwa Barcelona ikiwa na Ronald, anahitaji muda zaidi wa kuifanya timu iwe kwenye kiwango chake.



# TUCHEL HANA HOFU KUTIMULIWA PSG




**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amesisitiza hana shaka kuhusu majaliwa yake pale Paris Saint-Germain wakati kukiwa na uvumi kuhusu nafasi yake ya ukocha.

Nafasi ya Tuchel kama kocha wa miamba hao wa Ligue 1 imeibua maswali baada ya Jumanne kufungwa mabao 2-1 na Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mjerumani huyo alishinda taji la ligi na kuiongoza PSG kwenye fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa msimu wa 2019-20 kabla ya kufungwa na Bayern Munich.

Tuchel amepuuzia kuhusu majaliwa yake akiwaambia waandishi wa habari: "Siwezi kwenda kwenye Internet kutafuta jina langu kwenye Google. Najua namna gani mambo magumu hapa. Hilo ni sawa kwangu. Sitarajii chochote.

"Nasiwezi kufikiria namna presha ilivyokuwa nje ya dimba. Najua kwamba wengi wanaibua maswali nini kinaendelea.

"Sina wasiwasi wowote, kilichotokea ni sehemu ya mchezo, hivyo kuwapo au kutoendelea kuwapo hapa sio suala langu."

# *Al Ahly yatangulia fainali Afrika*

**CAIRO,** Misri

AL Ahly wamepata nafasi ya kurudi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Wydad Casablanca kwenye mchezo wa pili wa hatua ya nusu fainali.

Mabingwa hao mara nane walianza kuongoza mapema wakati wakiibuka na ushindi wa uwiano wa mabao 5-1 kwenye dimba la Cairo.

Kama walivyofanya kwenye mchezo wao wa kwanza, Al Ahly walipata bao la haraka la ufunguzi kupitia Marwan aliyeunganisha pasi ya Ahmed Tagnaouti dakika ya tano ya mchezo huo.

Hussein El Shahat alifunga goli la pili kwa miamba hao wa soka la Misri na Yasser Ibrahim akafunga bao la tatu.

Zouheir El-Moutaraji aliyetokea benchi alifunga bao la kufutia machozi kwa Wydad dakika ya 82 na halikutosha kuwafanya wafuzu kwenda kucheza fainali.

Al Ahly ambao walifungwa kwenye fainali mbili zilizopita, sasa inasubiri mshindi kati ya Zamalek au Raja Casablanca kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG ATETEWA KUHUSU KUTOKUFUNGA

Kocha wake ashangazwa na maswali yanayoulizwa juu ya mshambuliaji huyo ambaye...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alishangazwa na maswali juu ya namna anavyomtumia Pierre-Emerick Aubameyang huku mshambuliaji huyo wa Arsenal akiwa na wakati mgumu wa kufunga mabao kama ilivyokuwa msimu iliyopita.

**Aubameyang awali alikuwa akicheza kushoto chini ya Arteta, licha ya pia kuwa na nafasi kubwa kama mshambuliaji wa kati katika kipindi cha miaka miwili na nusu hapo kwenye dimba la Emirates.**

Tangu Februari 2018 kwenye Ligi Kuu England, ni Mohamed Salah pekee amefunga mabao mengi (60), kuliko nyota huyo wa kimataifa wa Gabon mwenye mabao 55.

Kabla ya kuanza kwa msimu huu mpya wa 2020-21, Aubameyang alikuwa na wastani wa kufunga baao kila baada ya dakika 124. Msimu huu mambo yamekuwa tofauti, kwani ana wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 450.

Alipoulizwa kama suluhisho la Aubameyang kumaliza ukame wa mabao ni kumchezesha katikati, Arteta alijibu: "Mara zote kuna maswali asipofunga, 'Kwanini asicheze namba tisa?' Na ukimchezesha namba tisa mtauliza, 'kwanini usimwache acheze kushoto kwa sababu amekuwa na mafanikio zaidi?' Hilo ndilo linalotokea, najua."

Aubameyang alishutumiwa kwenye mitandao ya kijamii wakati Arsenal ilipofungwa 1-0 na Manchester City wikiendi iliyopita, baada ya picha kumwonyesha akicheza na mchezaji nwenzake wa zamani wa Borussia Dortmund, Ilkay Gundogan mara baada ya mchezo huo.

"Matarajio ni makubwa kwake kwa sababu anafunga kila mechi, na hivyo asipofunga maswali yanaanza kuibuka," alisema Arteta kuhusu Aubameyang.

"Anatakiwa kukabiliana na hilo na sisi tupo hapa kwa ajili ya kumpa sapoti wakati ambapo anapitia kipindi kigumu."

Hadi sasa kwa mujibu wa mtandao wa Opta, Aubameyang bado hajafunga katika mechi kubwa kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Hata hivyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 alitokea benchi na kufunga bao la ushindi wa Arsenal wakati walipotoka nyuma na kuifunga Rapid Vienna kwenye Ligi ya Europa, Alhamisi.

## ZISIKUPITE

### SON APEWA MKATABA MNONO

TOTTENHAM Hotspur imempa ofa ya mkataba mpya wa miaka mitano fowadi wake raia wa Korea Kusini, Son Heung-min, 28, utakaomfanya kupokea mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki pamoja na bonasi ya kiwango bora, huku mkataba wake unamalizika 2023. ***(Football Insider)***

### MBAPPE ATAJWA MADRID

MPANGO wa Real Madrid kumsajili nyota wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 21, hautaathiriwa kama kocha Zinedine Zidane ataondoka klabuni hapo. ***(AS)***

### WAKALA AMTETEA OZIL

WAKALA wa nyota wa Arsenal, Mesut Ozil amedai kocha wa washikabunduki hao, Mikel Arteta, hakuwa na sababu ya maana ya kumwacha mchezaji huyo wa Ujerumani kwenye kikosi chake. ***(Guardian)***

### EMERSON KUONDOKA CHELSEA

BEKI wa kushoto wa Chelsea, Emerson Palmieri, 26, anaonekana anataka kuondoka wakati wa dirisha dogo la Januari, huku Inter Milan, Roma na Napoli zikionyesha nia ya kumwania. ***(Sky Sports Italia, via Express)***

### STEBANOVIC ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester City inapanga kumsajili winga wa Partizan, Filip Stevanovic, 18, kwa pauni milioni sita ifikapo Januari. Mchezaji huyo raia wa Serbia awali alikuwa akihusishwa na Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### PSG YAMGANDA NEYMAR

KLABU ya Paris St-Germain inapanga kuingia makubaliano ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar, 28. ***(Le10 Sport)***

### JORGINHO AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa Chelsea na Italia, Jorginho ,28, amesema "alifungua mlango wa majadiliano" na Arsenal na amekubali alikuwa akiwindwa na washikabunduki hao kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(ESPN Brazil)***

### BERTRAND MAMBO SAFI

MLINZI wa kushoto wa Southampton, Ryan Bertrand, mwenye umri wa miaka 31, anakaribia kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu. ***(Goal)***

### TARKOWSKI NJIA PANDA

BEKI wa Burnley na England, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 27, hakukaribia kusaini mkataba wa kujiunga na West Ham United wakati wa dirisha lililopita, kwa mujibu wa kocha, Sean Dyche. ***(Talksport)***

### ANGELINO AIKUMBUKA RB

BEKI wa kushoto wa Hispania, Angelino mwenye umri wa miaka 23, amesema hana tatizo la kutopata nafasi ya kucheza zaidi Manchester City, kwani kwa sasa anafikiria kurudi RB Leipzig. ***(Marca, via Inside Futbol)***

### BOLASIE AJIONGEZA

WINGA wa Everton na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Yannick Bolasie (31), atawasaidia nyota wapya walioko Liverpool ili kuwahakikishia wanapata nafasi ya kuendelea kufundisha. ***(Liverpool Echo)***

HABARI MICHEZO

## Nyota 22 Azam waifuata Mtibwa

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 22 wa Azam FC kiliwasili salama mjini Morogoro kwa ajili ya kuwavaa wenyeji Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani humo.

Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabit, alisema wachezaji wote walifika salama na leo wanatarajia kuendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo huo wa raundi ya nane.

Alisema wameenda Morogoro kwa kazi moja ya kuendeleza ushindi na wanaamini wachezaji watapambana ili kuhakikisha wanavuna pointi zote tatu.

Aliwataja wachezaji walioko katika msafara wa timu hiyo ni pamoja na Bennedict Haule, David Mapigano, Nicholas Wadada, Abdul Hamahama, Bruce Kangwa, Agrey Moris, Mudathir Yahya, Richard Djodi, Andrew Simchimba, Never Tigere, Frank Domayo, Abdallah Sebo na Ally Niyonzima.

Wachezaji wengine ni Iddy Nado, Daniel Amoah, Alan Thierry Akono Akono, Ayoub Lyanga, Yakubu Mohamed, Emmanuel Charles, Prince Dube, Obrey Chirwa na Salum Aboubakar 'Sure Boy'.

Azam FC ndio vinara wa Ligi Kuu Bara wakiwa na pointi 21 baada ya kushinda mechi zote saba walizocheza msimu huu, wakifuatiwa na Yanga yenye pointi 16 na Simba yenye pointi 13, lakini vigogo hao wa soka nchini wakicheza mechi moja pungufu.

## Igunga wahitaji uwanja wa kisasa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MGOMBEA Ubunge mteule wa Jimbo la Igunga Mjini kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Nicholaus Ngassa, amesema endapo atapata ridhaa ya kuliongoza jimbo hilo ataipa kipaumbele sekta ya michezo.

Akitangaza vipaumbele vyake 10 kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya CCM Mjini Igunga, Ngassa alisema atahakikisha sanaa na utamaduni zinafanya vyema chini ya uongozi wake.

Ngassa aliahidi endapo atashinda kiti hicho, ataandaa bonanza la michezo litakalofanyika Desemba, mwaka huu kwa kushindanisha mchezo wa soka na netiboli kwa wanaume na wanawake.

Naye mmoja wa wadau wa michezo katika jimbo hilo, Ibrahimu Saidi, licha ya kuupongeza mpango wa sekta ya michezo, alitoa ushauri wake kwa kumtaka mgombea huyo kutafuta wadhamini wa kujenga uwanja wa kisasa wa michezo.

Ibrahimu alisema endapo watapata uwanja wa michezo, wanaamini uchumi wa wilaya hiyo utaongezeka kwa sababu michezo huchangia kukuza biashara.

Beatrice Mnyambo alisema endapo mbunge huyo atashinda na kutimiza ndoto zao za kuwajengea uwanja, watampa ushirikiano katika muda wake wote wa uongozi.

Mnyambo alisema michezo itatumika kuwaunganisha vijana wa jimbo hilo na itaimarisha upendo, mshikamano na itasaidia kujenga na kulinda afya zao.

# TSHISHIMBI APATA ULAJI AS VITA CONGO

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa zamani wa Yanga, Papy Tshishimbi, ametia saini mkataba wa mwaka mmoja na klabu ya AS Vita Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

**Akizungumza na gazeti hili jana, Tshishimbi alisema ameamua kutia saini mkataba wa mwaka mmoja tu kwa sababu hapendi kucheza soka katika ardhi ya nyumbani kwao.**

"Ni kweli nimesaini AS Vita ya nchini kwetu, wao walitaka nisaini mkataba wa miaka miwili, lakini mimi nimekataa, nimewaambia nataka nisaini mwaka mmoja. Unajua mimi sipendi sana kucheza soka huku kwetu, kwa sababu ukicheza soka nyumbani hata heshima inakuwa hakuna, unachukuliwa kama ni mchezaji wa kawaida tu, dharau inakuwa nyingi," alisema Tshishimbi.

Kiungo huyo alisema alisaini mkataba huo siku ya Jumatano na kwa sasa anasubiri kibali cha uhamisho wa kimataifa ITC kutoka Tanzania ili aanze kuitumikia timu hiyo mpya.

"Kama kibali kitatumwa mapema, basi nitacheza mechi ya Jumapili (leo), tunacheza dhidi ya FC Lupopo, lakini kama ikishidikana na ikachelewa, basi nitacheza mechi ya Jumatano ambayo itakuwa dhidi ya Blessing FC," Tshishimbi alisema.

Tshishimbi aliachana na Yanga mwishoni mwa msimu uliopita baada ya kushindwa kuelewana dau la usajili na klabu yake ikatangaza kutoendelea naye.

Mchezaji huyo alijiunga na Yanga mwaka 2017, akitokea Mbabane Swallows ya nchini Swaziland.

Kabla ya kwenda kurudi kwao, klabu za Simba na Azam zilihusishwa kuwania saini ya Mkongomani huyo.

Wakati Tshishimbi akisaini mkataba wa AS Vita, klabu hiyo yenyewe iliwauza viungo wake, Mukoko Tonombe na Tusila Kisinda kwenda Yanga.

Hata hivyo, mpaka sasa Tshishimbi bado hajacheza mechi yoyote, tayari Tonombe ana mabao mawili mpaka sasa akiwa Yanga, na kuifanya timu hiyo kuwa kwenye nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 16, huku AS Vita yenye pointi saba iko kwenye nafasi ya tatu.



Mshambuliaji wa Yanga, Yacouba Sogne (katikati), akijaribu kuwatoka wachezaji wa Polisi Tanzania waliomzunguka katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa hivi karibuni kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Lipuli Day kufanyika kesho Iringa*

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

UONGOZI wa Lipuli unatarajia kutambulisha rasmi jezi yake mpya watakayoitumia katika msimu wa 2020/21 wa Ligi Daraja la Kwanza kwenye tamasha la klabu hiyo "Lipuli Day" litakalofanyika kesho kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani hapa.

Mwenyekiti wa Lipuli, Ayubu Kiwele, alisema maandalizi ya tamasha hilo yamekamilika na wanawaomba mashabiki na wadau wa soka wa Iringa kujitokeza kuangalia mikakati iliyopangwa na klabu yao.

Kiwele alisema wanaishukuru Kampuni ya Vunjabei ambayo ilikubali kuingia udhamini wa mwaka mmoja, ambao utawafanya wapate vifaa mbalimbali vya michezo ikiwamo jezi.

"Tumejipanga kufanya vizuri katika Ligi Daraja la Kwanza, hatutaki kurudia makosa, tunaahidi tutarejea tena Ligi Kuu Bara msimu ujao," alisema kiongozi huyo.

Kiwele alisema kampuni hiyo pia itauza jezi za timu yao katika maduka yake yote na klabu itapata mgawo wake kulingana na makubaliano ambayo wamefikia.

Naye Meneja wa Kampuni ya VunjaBei, Fadhili Ngajilo, aliishukuru klabu hiyo kwa kukubali kushirikiana nao na wameahidi kuisaidia ili irejee katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumesaini mkataba wa mwaka mmoja na Kampuni ya Vunjabei, mkataba huo unahusisha pia kuuza jezi za Lipuli. Zinapatikana kwa Sh. 20,000. Kwa Iringa duka lipo Uhindini. Timu hiyo tumeidhamini kwa kuipa vifaa na jezi kwa msimu wote wa ligi," alisema Ngajilo.

Kabla ya kushuka daraja, iliichukua miaka 17 kwa Lipuli kurejea tena katika Ligi Kuu Bara ambayo bingwa wake hushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mbali na Lipuli, timu nyingine kutoka Ligi Kuu Bara zilizoshuka daraja ni pamoja na Singida United, Alliance FC, Ndanda FC na Mbao FC.

# Michezo

Jumapili Oktoba 25, 2020

Nipashe




Aubameyang atetewa kuhusu kutokufunga


URASA 22


# Yanga majaribuni Mwanza

## ●●● Ni katika vita nyingine ya kuwania pointi tatu muhimu za Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC...

**Na Somoe Ng'itu**

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea kwa wenyeji KMC FC kutoka Dar es Salaam kuwakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wamejipanga kuongeza umakini kutokana na rekodi nzuri na wapinzani wao msimu huu.**

Kaze (pichani) alisema bado anaendelea kukijenga vyema kikosi chake, hivyo baadhi ya idara zinaendelea kuimarika taratibu, lakini wataingia uwanjani wakiwa na malengo ya kusaka ushindi na si matokeo mengine.



Mrundi huyo alisema anafurahi kuona ushindani wa namba na juhudi zinazoonyeshwa na wachezaji wa timu hiyo ambao pia wanahitaji kufanya vizuri katika kila mechi watakayocheza.

"Katika soka hakuna mechi rahisi, hakuna mechi nyepesi, ila mechi zote ni muhimu, tumejiandaa kupata matokeo mazuri, pointi tatu ni muhimu huku kikosi kikiendelea kuonyesha ubora," alisema Kaze.

Kocha huyo aliwataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kuendelea kuimarisha umoja ili kuwaongezea nguvu wachezaji wao ambao wanaingia uwanjani kupambana.

"Asante Yanga, tulianza vizuri na ninatumaini Jumapili tutakuwa pamoja, tumejipanga na tunategemea ushindi," Kaze aliongeza.

Kocha wa KMC, Habib Kondo, maandalizi kuelekea mchezo wa leo yamefanyika vizuri na walifika jijini Mwanza mapema ili kujiweka tayari kuikabili Yanga.

Kondo alisema wamekwenda Mwanza kwa sababu moja tu ya kusaka ushindi lakini watashuka uwanjani wakiwa wanawaheshimu wapinzani wao.

"Tuna siku tatu hapa Mwanza, tumekamilisha maandalizi yetu leo( jana)kuelekea mchezo huo, tuko tayari kwa ajili ya kupambana ili kupata pointi, tunaufikiria zaidi mchezo huu na michezo iliyopita haiko katika mipango yetu," alisema Kondo.

Kocha huyo aliongeza kila mechi ina mikakati yake, hivyo wameshasahu matokeo ya mechi zilizopita na sasa wanaiangalia Yanga ambayo hawaihofii.

"Michezo iliyopita imeshapita, wao walicheza na Polisi Tanzania na sisi tulicheza mechi yetu, japokuwa Yanga ni timu kubwa, timu

Alisema hana mchezaji ambaye ni majeruhi na kila nyota aliyeko Mwanza yuko tayari kupambana kuondoka na ushindi.

"Tumekuja Mwanza kusaka pointi tisa katika mechi zetu tatu, tunaanza na Yanga, halafu tunaenda kuchukua kwa Gwambina na Biashara, baada ya hapo tutarejea Dar es Salaam na tutarudi kwa kishindi kutokana na ushindi ambao tutakuwa tumepata kwenye mechi hizo," Kondo alisema.

Wakati huo huo, katika mechi ya mapema jana mchana, Ihefu FC ilipata sare ya bila kufungana na Namungo FC katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.



Kiungo mkabaji wa West Ham, Tomas Soucek (kushoto), akijipanga kumzuia mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba kumaliza hasira kwa Ruvu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata kichapo katika mchezo uliopita, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wamesema watamaliza 'hasira' za kufungwa watakapowakaribisha Ruvu Shooting hapo kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kilianza mazoezi jana na kila mchezaji ameahidi kujirekebisha kuelekea mchezo huyo wa raundi ya nane.

Rweyemamu alisema wanafahamu kila mechi ya ligi ni muhimu, hivyo wataongeza umakini katika mechi ya leo kwa sababu malengo yao ni kutetea taji hilo wanalolishikilia.

"Ukimaliza mechi unafunga hesabu, huwezi kubadilisha matokeo, unaanza ukurasa mpya, sasa hivi kiufundi tunaangalia Ruvu Shooting, ndio mtihani ulioko mbele yetu, tumeshaanza kuipigia hesabu, tujue tutamalizana nao vipi," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo alisema wachezaji waliokuwa majeruhi wanaendelea vyema na kila mmoja anafanya mazoezi kulingana na programu aliyopewa na daktari.

"Watarudi, siwezi kusema lini, lakini kuna matumaini ya mapema, hakuna mwenye tatizo kubwa hadi sasa, mashabiki watawaona hivi karibuni," Rweyemamu aliongeza.

Mabingwa hao watetezi wana pointi 13, wameshinda mechi nne, wametoka sare mara moja na wamepoteza mchezo mmoja dhidi ya Tanzania Prisons Alhamisi iliyopita wakiwa ugenini kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga, Rukwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >